Haliuzwi
APRIL 7, 2026
/islamicftz
Shawwal 19 1447

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 577

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Libya, Kenya zang'ara Mashindano ya Dunia ya Qur'an Dar



# Imam Al-Turki ausia kushikamana na Qur'an

- Juhudi za Rais Mwinyi kuendeleza masuala ya dini ya Kiislamu nchini zampa tuzo mbili za heshima





## Saudi Arabia yaimarisha maandalizi ya msimu wa Hija

## Presha ya mafuta yaisukuma LATRA, wadau wa sekta ya usafiri kukutana

**Wakati bei za mafuta zikifikia viwango vya juu zaidi kuwahi kushuhudiwa, Latra inatarajiwa kukutana na wadau wa sekta ya usafiri kesho, Aprili 8, 2026, kujadili marekebisho ya nauli na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.**




## Waziri wa Fedha: Afrika ijipange kukabili athari za migogoro ya dunia

## Amani itadumu Uislamu ukitawala dunia

شَوَّال

HABARI
DAR ES SALAAM

NA SARA ZUBERI

# Imam Al-Turki ausia kushikamana na Qur'an




Imam wa Msikiti Mtakatifu wa Makka, Sheikh Dkt. Badr Al–Turki, ametaka kuwapo kwa juhudi za pamoja baina ya walimu na wazazi katika kuwasomesha na kuwahifadhisha watoto Qur'an Tukufu.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuhuisha amani na utulivu, na hivyo kuijengea Tanzania heshima na hadhi duniani.

Sheikh Al–Turki alitoa kauli hiyo wakati wa Mashindano ya Dunia ya 34 ya Kuhifadhi Qur'an Tukufu yaliyofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Alieleza kuwa Qur'an ina mchango mkubwa katika kuwaandaa raia wema, akisisitiza kuwa mtu anayeijua Qur'an kwa kiwango cha kushindana katika kuhifadhi hawezi kuwa na tabia mbaya kwa kuwa moyoni mwake kuna hofu ya Allah.

Awali, mwakilishi wa Waziri wa Masuala ya Dini, Da'awah na Muongozo wa Saudi Arabia, Sheikh Muhammad Al–Arifi, alipongeza ushirikiano wa Tanzania na Saudi Arabia, akisema kuwa umeimarisha zaidi uhusiano baina ya mataifa hayo mawili.

Pia aliwashukuru wale wote wanaosimamia mashindano ya kusoma na kuhifadhi Qur'an hapa nchini, akibainisha kuwa yanachangia kuimarisha umoja na mshikamano wa Kiislamu.

## Wasifu wa Sheikh Badr Al–Turki

Sheikh Badr Al–Turki ni mmoja wa maimamu wa Msikiti Mtakatifu wa Makka, nafasi aliyoteuliwa kuishika tangu mwaka 2024 akiwa na umri wa takriban miaka 40, hivyo kuwa miongoni mwa maimamu vijana zaidi kuhudumu katika Msikiti huo muhimu katika Uislamu.

Sheikh Al–Turki alizaliwa Agosti 21, 1984 jijini Riyadh, Saudi Arabia, ambako pia alipata malezi na msingi wa elimu ya dini ya Kiislamu. Kabla ya kuteuliwa kuwa Imam wa Makka aliwahi kuwa Imam na khatibu katika Msikiti wa Prince Bandar bin Abdulaziz mjini Riyadh, ambako alijulikana kwa usomaji mzuri wa Qur'an na uongozi mzuri katika shughuli za kidini.

Kielimu, Sheikh Al–Turki ana Shahada ya Kwanza (B.A.) katika Da'wah kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhammad ibn Saud. Pia alipata Shahada ya Uzamili (M.A.) katika Da'wah, na kwa sasa anaendelea na masomo ya Shahada ya Uzamivu (PhD) katika fani hiyo.

Kutokana na elimu yake, uwezo wa uongozi na umahiri katika kusoma Qur'an, aliteuliwa kuwa Imam wa Msikiti wa Makka na kujiunga na kundi la maimamu wachache wanaoongoza ibada katika moja ya misikiti Mitakatifu zaidi katika Uislamu.

شوّال

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA SARA ZUBERI




# Libya, Kenya zang'ara Mashindano ya Dunia ya Qur'an Dar es salaam

Washiriki kutoka Libya na Kenya wameibuka washindi wa kwanza katika makundi mawili tofauti ya mashindano ya kimataifa ya kusoma Qur'an Tukufu yaliyofanyika Aprili 5, 2026 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, yakishirikisha takribani washindani kutoka nchi 26 duniani.

Katika kundi la washiriki wakubwa, mshindi wa kwanza alikuwa Ibrahim Hilal kutoka Libya, aliyepata alama 99.12 na kujinyakulia zawadi ya dola za Marekani elfu nane, sawa na takribani Shilingi milioni 20 za Tanzania.

Nafasi ya pili ilichukuliwa na Said Said kutoka Mauritania, huku nafasi ya tatu ikienda kwa Ahmed Karim kutoka Urusi.

Kwa upande wa kundi la watoto wenye umri wa miaka nane hadi 12, mshindi wa kwanza alikuwa Mohamed Said Ahmed Zamzam mwenye umri wa miaka 10 kutoka Kenya, aliyepata alama 97.43 na kujishindia dola elfu nane.

Ukiacha Zamzam, aliyetajwa kuiwakilisha vema Afrika ya Mashariki, nafasi ya pili katika kundi la watoto ilichukuliwa na mshiriki kutoka Comoro, wakati nafasi ya tatu ikienda kwa Ahmad Tamer kutoka Misri.

Mashindano hayo yalihudhuriwa na maelfu ya watazamaji na yalionogeshwa zaidi na zawadi mbalimbali kwa waliohudhuria, zikiwemo bodaboda kumi pamoja na tiketi tatu za kwenda Hijja zilizotolewa kwa washiriki wa bahati nasibu.

## Imam wa Makka anogesha

Tukio hilo pia lilipambwa na ujio wa ujumbe maalumu kutoka Saudi Arabia ukiongozwa na Imamu wa Msikiti Mtakatifu wa Makka, Imam Badr Al Turki.

Al Turki, aliyewasili siku ya Jumamosi, alipokelewa na Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, pamoja na viongozi wengine wa Kiislamu na kamati ya maandalizi ya mashindano hayo.

Akiwa jijini Dar es Salaam, Imam Badr Al Turki alipata fursa ya kutoa mhadhara katika Msikiti wa Mtoro, Kariakoo, ambako alihimiza Waislamu kujenga tabia ya kuwa na marafiki wema, akieleza kuwa rafiki ana nafasi kubwa katika kumsaidia mtu kufuata njia sahihi au kumpotosha.

Alifafanua kuwa rafiki mwema ni kama muuzaji wa uturi, akimaanisha kuwa ukikaa karibu naye utanufaika na tabia njema. Aidha, alisisitiza umuhimu wa kutafuta elimu, hususan elimu ya dini, akieleza kuwa elimu humuinua mtu duniani na akhera na kumsaidia kumjua vizuri Mwenyezi Mungu.

Katika mawaidha yake, pia aliwahimiza Waislamu kujifunza kusoma Qur'an, kuihifadhi, kuitafakari na kuitekeleza, pamoja na kuwafundisha wengine hususan familia zao.

NA SARA ZUBERI

# Presha ya mafuta yaisukuma LATRA, wadau wa usafiri kukutana

**Kwa sasa, petroli inauzwa kwa Sh3,820 kwa lita kutoka Sh2,864 mwezi Machi—ongezeko la asilimia 33.4. Dizeli imepanda hadi Sh3,806 kutoka Sh2,858, huku mafuta ya taa yakifikia Sh3,684 kutoka Sh2,932.**

Wakati bei za mafuta zikifikia viwango vya juu zaidi kuwahi kushuhudiwa, Land Transport Regulatory Authority (Latra) inatarajiwa kukutana na wadau wa sekta ya usafiri kesho, Aprili 8, 2026, kujadili marekebisho ya nauli na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Kwa sasa, petroli inauzwa kwa Sh3,820 kwa lita kutoka Sh2,864 mwezi Machi—ongezeko la asilimia 33.4. Dizeli imepanda hadi Sh3,806 kutoka Sh2,858, huku mafuta ya taa yakifikia Sh3,684 kutoka Sh2,932.

Ongezeko hilo linatokana na uvamizi wa United States na Israel dhidi ya Iran Februari 28, 2026, pamoja na kuzuiwa kwa njia ya Strait of Hormuz na mataifa hasimu. Hali hii imevuruga usambazaji wa mafuta duniani, na kusukuma bei ya mafuta ghafi kupanda zaidi ya dola 100 kwa pipa, huku Brent ikiuza kati ya dola 105 hadi 110.

Kupanda huku kumeongeza presha kwa sekta ya usafiri inayotegemea sana mafuta katika uendeshaji wa kila siku. Kwa ujumla, bei kubwa za mafuta hufanya kama kodi isiyo ya moja kwa moja kwa watumiaji na wafanyabiashara, kupunguza kipato kinachoweza kutumika, kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuongeza mfumuko wa bei.

Wamiliki wa mabasi, bajaji na pikipiki wanatarajiwa kuwasilisha mapendekezo yao ya marekebisho ya nauli katika kikao hicho cha Latra. Majadiliano pia yataangazia gharama za uendeshaji, changamoto za utoaji huduma na hatua za udhibiti ili kuhakikisha sekta inaendelea kufanya kazi licha ya kupanda kwa bei za mafuta.

Katibu Mkuu wa Tanzania Bus Owners Association, Bw. Priscus Joseph, amesema ongezeko la nauli haliepukiki lakini linapaswa kuwa la wastani na kuzingatia gharama halisi.

"Nauli ziongezwe baada ya mahesabu sahihi. Baadhi ya waendeshaji wamepandisha nauli kupita kiasi, jambo linalowaumiza abiria," alisema.

Wakati huohuo, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Association of Oil Marketing Companies, Raphael Mgaya, ameonya kuwa wananchi wanapaswa kujiandaa na ongezeko zaidi la bei za mafuta. Amesema bei za sasa zinatokana na mafuta yaliyoagizwa awali, na mzigo ujao unaweza kuongeza bei zaidi.

Pia alipendekeza taasisi zinazoweza kuruhusu wafanyakazi kufanya kazi kwa mbali zifanye hivyo ili kupunguza matumizi ya mafuta. "Mwezi ujao bidhaa nyingi zitapanda bei kadri mafuta yanavyozidi kupanda. Hii ni hali isiyo ya kawaida inayohitaji mipango na ushirikiano," alisema.

## Nafasi ya Latra

Kadri Land Transport Regulatory Authority inavyoitisha kikao hicho, wadau wanatarajiwa kupima hitaji la haraka la kurekebisha nauli dhidi ya athari pana za kiuchumi. Wachambuzi wanasisitiza umuhimu wa uratibu wa pamoja kulinda walaji, kusaidia waendeshaji na kudumisha utulivu wa sekta ya usafiri.

Kikao hicho kinatarajiwa kuwakutanisha viongozi wa serikali, wamiliki wa mabasi na malori, waendesha bajaji na pikipiki pamoja na wadau wengine, kujadili hatua za muda mfupi na mikakati ya muda mrefu ya kukabiliana na athari za kupanda kwa bei za mafuta.

Katika wiki zijazo, wananchi na wafanyabiashara watafuatilia kwa karibu matokeo ya kikao hicho, ambacho kinaweza kuweka mwelekeo wa namna Tanzania itakavyokabiliana na kipindi kigumu katika sekta ya usafiri na usafirishaji.



NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi apokea tuzo za heshima kwa kukuza masuala ya Kiislamu



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa mashindano ya kuhifadhi Qur'an yamekuwa chachu ya kuibua vipaji vya vijana pamoja na kukuza maadili mema katika jamii.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo tarehe 05 Aprili 2026, katika dhifa ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na Jumuiya ya Tuzo za Kimataifa za Kuhifadhi Qur'an Tukufu, iliyofanyika katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Ameeleza kuwa mashindano ya kuhifadhi Qur'an siyo tu mashindano ya Kitabu Kitukufu, bali pia ni kielelezo cha kuitambulisha Tanzania yenye amani duniani kote.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi ameishukuru Taasisi ya Tuzo za Kuhifadhi Qur'an Tanzania chini ya uongozi wa Sheikh Othman Ali Kaporo kwa kuendeleza mashindano hayo kwa mafanikio, pamoja na kuandaa dhifa hiyo ya chakula cha usiku kwa washiriki.

Miongoni mwa waliohudhuria hafla hiyo ni mgeni maalum, Sheikh wa Msikiti wa Al-Haram wa Makkah, Sheikh Badr bin Muhammad Al-Turki, pamoja na Balozi wa Saudi Arabia nchini. Mhe. Yahya Bin Ahmed Okeish.

Mashindano ya Kimataifa ya Kuhifadhi Qur'an yamefanyika tarehe Leo 5 Aprili 2026 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo mshiriki kutoka Libya, Ibrahim Hilal Zeydaan, amekuwa mshindi wa kwanza kwa kupata pointi 99.12. Mshindi wa pili ni Saydina Al Ghalla kutoka Mauritania aliyepata pointi 99.06, na mshindi wa tatu ni Ahmed Karim Shehmadduf kutoka Urusi aliyepata pointi 98.75.

Kwa upande mwingine Rais Dkt. Mwinyi ametunukiwa tuzo mbili maalum za kutambua juhudi na mchango wake katika kuendeleza masuala ya dini ya Kiislamu nchini, zilizotolewa na Ubalozi wa Saudi Arabia na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Tanzania.

شَوَّال

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Amani itadumu Uislamu ukitawala dunia



Waziri Mkuu wa Malaysia, Malaysia, Mheshimiwa Dato' Sri Anwar Ibrahim (kushoto), akiwa na Sheikh Dkt. Mohammed Al-Issa, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kiislamu Duniani Ikulu ya Taifa mjini Kuala Lumpur, mji mkuu wa Malaysia

Waziri Mkuu wa Malaysia, Anwar Ibrahim, amesema nchi yake inashikilia msimamo kwamba migogoro yote ya Mashariki ya Kati inapaswa kutatuliwa kwa njia za amani ili kupunguza mvutano unaozidi kuongezeka katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa Anwar, mazungumzo, diplomasia na ushirikiano wa karibu kati ya mataifa ndiyo njia pekee ya kupunguza mvutano huo na kurejesha utulivu, kwa kuzingatia mahitaji ya kibinadamu pamoja na kanuni za haki kwa wote.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa mazungumzo kwa njia ya simu mnamo Machi 24, 2026, na Mwanamfalme na Waziri Mkuu wa Bahrain, Salman Hamad Al–Khalifa, pamoja na Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Sheikh Mohammed Zayed Al–Nahyan.

Ndugu zangu katika imani, mimi si shabiki wa misimamo mikali, lakini ninathamini watu wanaotazama mambo kwa uhalisia wake. Hivyo, ni vyema kujiuliza kama kauli ya Anwar Ibrahim inafaa kutolewa na kiongozi wa nchi ya Waislamu katika wakati kama huu.

Je, ni sahihi kutegemea mazungumzo, diplomasia na ushirikiano na adui anayewaua kinyama Waislamu, anayevamia ardhi zao na kuitukana dini yao? Je, mauaji ya zaidi ya Waislamu 70,000 kule Gaza pamoja na uharibifu mkubwa, sambamba na mauaji yaliyotokea Syria na Yemen, hayatoshi kuthibitisha kuwa hawa ni maadui wasioweza kuelewa lugha ya diplomasia?

Kauli hii inaonekana kujitenga na uhalisia, na pia inapingana na maagizo ya Jihad yanayopatikana kwa wingi ndani ya Qur'an Tukufu na hadith za Mtume.

Uhalisia uliopo ni kwamba, ndugu zetu wanashambuliwa na ardhi zao zinavamiwa. Ni muhimu kujiuliza endapo Malaysia ingekumbwa na uvamizi na raia wake kuuawa kinyama huku ardhi yao ikitekwa, je wangechagua mazungumzo na ushirikiano na adui kusaka amani?

Iwapo wavamizi wangetaka kuvunja nguvu zao za kijeshi, kupora rasilimali zao, kuwafukuza kwenye makazi yao na kuondoa uhuru wao, je wangealikwa kwenye meza ya mazungumzo ili kujadili amani?

Kwa hakika, watu waoga, wajinga na wasaliti ndiyo wanaoweza kushirikiana na adui katika mazingira kama hayo, wakikabidhi rasilimali za nchi yao, kuruhusu taifa lao liangamizwe na ndugu zao kuuawa.

Mwenyezi Mungu tayari ametupatia mwongozo na suluhisho la namna ya kukabiliana na adui anayepigana nasi – si kwa mazungumzo, diplomasia wala ushirikiano. Anasema: "Na piganeni katika Njia ya Allah na wale wanaokupigeni..." [Qur'an, 2:190].

MAHMOUD NYAMGUMA




# Mufti Uganda awataka Waislamu kuandika wasia zao

Mufti wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, amewataka Waislamu kuweka kipaumbele katika kuandika wasia wao binafsi ili kuepusha migogoro ya kifamilia na kuhakikisha mali zao zinagawanywa kwa utaratibu unaokubalika kidini.

Akinukuliwa na tovuti ya Nile Post katika hafla moja ya kidini, Mufti Mubaje alisema kuandika wasia ni jukumu muhimu kwa Muislamu na ni sehemu ya mafundisho ya dini ya Kiislamu.

Alieleza kuwa baadhi ya watu wanaogopa kuandika wasia wakidhani ni ishara ya kifo kinachokaribia, lakini akasisitiza kuwa kufanya hivyo ni hatua ya busara inayosaidia kupanga vyema masuala ya familia na mali baada ya mtu kufariki. Mufti huyo aliwahimiza waumini kuhakikisha wanaandika matakwa yao kuhusu familia na mali zao kabla ya kulala, akisisitiza kuwa maisha ya mwanadamu ni ya muda mfupi na kila mtu anapaswa kujiandaa kwa maisha ya Akhera.

Mufti Mubaje aliwataka Waislamu kuishi maisha ya uchamungu, kuendelea kumuabudu Mwenyezi Mungu na kudumisha maadili mema katika jamii.

# Wakenya wahimizwa kuzingatia uwekezaji fedha zao kimaadili

Wawekezaji nchini Kenya wanapaswa kuanza kuzingatia si tu faida na hatari za uwekezaji bali pia maadili yanayoongoza matumizi ya fedha zao, amesema mchambuzi wa masuala ya uwekezaji Abdullahi Adan.

Katika makala ya maoni yenye kichwa “Why values-based investing matters for Kenyan savers” iliyochapishwa na Business Daily Africa, Adan anasema wawekezaji wengi nchini Kenya huzingatia zaidi kiwango cha faida na hatari wanazokabiliana nazo, lakini hawajiulizi fedha zao zinawekezwa katika shughuli zipi.

Adan, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Islamic Investment Banking (SIB Najah) katika Standard Investment Bank, anaeleza kuwa duniani kote wawekezaji wanaanza kutambua kuwa namna fedha zinavyowekezwa ni muhimu sawa na faida inayopatikana.

Mwelekeo huo umechochewa na kuongezeka kwa uwekezaji unaozingatia misingi ya mazingira, jamii na utawala bora (ESG), ambao sasa unaathiri mabilioni ya dola katika masoko ya fedha duniani. Aidha, sekta ya fedha za Kiislamu – mojawapo ya mifumo ya uwekezaji unaozingatia maadili – imekua na kufikia zaidi ya dola trilioni tatu duniani.

Kwa mujibu wa Adan, tafiti za taasisi za kimataifa kama MSCI na Morningstar zinaonyesha kuwa uwekezaji unaozingatia maadili unaweza kutoa matokeo yanayolingana au hata kuzidi uwekezaji wa kawaida katika muda mrefu.

Makala hiyo inaeleza kuwa uwekezaji unaozingatia maadili unaweza pia kusaidia kupunguza hatari kwa kuwa kampuni zinazoendeshwa kwa uwazi na uwajibikaji huwa na uwezo mkubwa wa kudumu katika muda mrefu. Pia, kwa kuwa mitaji ya kimataifa inavyoelekezwa zaidi katika masoko yenye uwazi na uwajibikaji, Kenya inahitaji kuimarisha mifumo ya uwekezaji unaozingatia maadili ili kuvutia wawekezaji na kukuza uchumi.

Anaongeza kuwa kadri Kenya inavyoendeleza mifumo ya uwekezaji mbadala na fedha za Kiislamu, wawekezaji wanapaswa kujiuliza swali muhimu: fedha zao zinachangia kujenga uchumi wa aina gani na zinasaidia shughuli zipi katika jamii.

شوّال

# HABARI ZA MISIKITI MITAKATIFU

MAHMOUD NYAMGUMA

# Saudi Arabia yaimarisha maandalizi ya msimu wa Hija



Saudi Arabia imeongeza kiwango cha maandalizi kwa ajili ya msimu wa Hija wa mwaka huu huku viongozi wa ngazi ya juu wakifanya mikutano ya tathmini ya mipango ya kiutendaji na huduma kwa mahujaji.

Kwa mujibu wa Saudi Gazette na Asharq Al-Awsat, Waziri wa Hija na Umrah, Tawfiq Al-Rabiah, amefanya mfululizo wa mikutano na wawakilishi wa nchi mbalimbali pamoja na kampuni na taasisi zinazohusika na huduma za mahujaji ili kuimarisha ubora wa huduma na uratibu wa wadau katika mfumo wa Hija na Umrah.

Mikutano hiyo ilifanyika pembezoni mwa Jukwaa la Umrah na Ziyara lililofanyika Madinah, kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri, malazi na huduma nyingine kwa wageni wa Nyumba Takatifu, kwa mujibu wa Saudi Gazette.

Wakati huohuo, mamlaka za Saudi zimepitia kwa kina kiwango cha maandalizi ya msimu wa Hija katika mikutano ya Kamati ya Kudumu ya Hija na Umrah vikiongozwa na Naibu Emir wa Makkah, Princ Saud bin Mishaal bin Abdulaziz na Emir wa Madina, Prince Salman bin Sultan bin Abdulaziz.

شوّال

# HABARI ZA MISIKITI MITAKATIFU

MAHMOUD NYAMGUMA

# Uwanja mpya wa ndege kuwezesha mahujaji kutua Makkah moja kwa moja



Saudi Arabia imeidhinisha mipango ya kujenga uwanja mpya wa ndege pamoja na mfumo wa metro mjini Makkah katika juhudi za kuboresha usafiri na huduma kwa mamilioni ya mahujaji wa Hija na Umrah wanaofika kila mwaka.

Uwanja huo, ukijengwa, utawezesha mahujaji kutua Makkah moja kwa moja badala ya aghlabu Jeddah uwanja wa King Abdulaziz International Airport (JED) ulioko takriban kilomita 70–90, kiasi cha mwendo wa saa moja hadi saa moja na nusu kwa gari. Uwanja huo una moja ya temino kubwa zaidi duniani, maalumu kwa mahujaji,

Akinukuliwa na tovuti za The Pakistan Connect na Siasat, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Kifalme ya Mji wa Makkah na Maeneo Matakatifu, Saleh Al-Rasheed, alisema mipango ya kimkakati na uwekezaji wa mradi huo tayari imepitishwa ili kujenga uwanja wa ndege utakaofikia viwango vya kimataifa na kuongeza uwezo wa kuhudumia wageni wa Nyumba Takatifu. Alisema ujenzi wa mradi huo utafanyika kwa ushirikiano na sekta binafsi ili kuunda mifumo bora ya uwekezaji bila kuathiri ufanisi wa viwanja vingine vya ndege vilivyo karibu.

Aidha, tafiti za uwezekano na michoro ya awali ya mradi wa Makkah Metro tayari zimekamilika, hatua inayolenga kuimarisha usafiri wa ndani na kuunganisha maeneo muhimu ya ibada. Mamlaka pia zimeanzisha programu ya "Smart Makkah" inayotumia akili mnemba (AI) kufuatilia na kudhibiti msongamano wa watu katika maeneo kama Msikiti Mkuu wa Makkah na daraja la Jamarat.

Miradi hiyo ni sehemu ya juhudi za Saudi Arabia kuboresha miundombinu na kuongeza ubora wa huduma kwa mahujaji.

## Jukwaa la Umrah na Ziyarah lakamilika Madinah

**Madinah — Toleo la tatu la Jukwaa la Umrah na Ziyarah limehitimishwa Jumatano mjini Madinah baada ya siku tatu za majadiliano na maonesho yaliyolenga kuboresha huduma kwa mahujaji na wageni wanaotembelea maeneo matakatifu katika kuunga mkono malengo ya Dira ya Saudi 2030.**

**Jukwaa hilo lilifanyika kuanzia Machi 30 hadi Aprili 1 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha King Salman, chini ya udhamini wa Gavana wa Mkoa wa Madinah, Prince Salman bin Sultan bin Abdulaziz, na kuandaliwa na Wizara ya Hija na Umrah kwa ushirikiano na Mpango wa Uzoefu wa Mahujaji. Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Saudi (SPA), tukio hilo lilivutia zaidi ya washiriki 50,000 kutoka nchi 165, likiimarisha hadhi yake kama jukwaa la kimataifa la kuendeleza huduma za Umrah na ziara za kidini huku mikataba na makubaliano ya ushirikiano 5,400 ikitiwa saini kati ya taasisi za serikali, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali - ongezeko la zaidi ya asilimia 25 toka toleo lililopita.**

## Msikiti wa Al-Aqsa wafungwa kwa wiki 5 mfululizo

**Jerusalem — Msikiti wa Al-Aqsa ulioko Jerusalem Mashariki umeendelea kufungwa kwa wiki 5 mfululizo kufuatia hali ya tahadhari ya kitaifa iliyotangazwa na Israel wakati wa operesheni ya kijeshi inayohusisha Israel na Marekani dhidi ya Iran.**

**Kwa mujibu wa Arab News, mamlaka za Israel zimepiga marufuku mikusanyiko mikubwa katika maeneo matakatifu ya Jerusalem, hatua iliyosababisha kufungwa kwa maeneo ya ibada ikiwemo Msikiti wa Al-Aqsa.**

**Mamlaka ya Palestina imelaani uamuzi huo na kueleza wasiwasi kuhusu wito wa walowezi wenye misimamo mikali wanaotaka kuruhusiwa kuingia katika eneo la msikiti huo kufanya ibada.**

**Msikiti wa Al-Aqsa unasimamiwa kisheria na Wizara ya Wakfu ya Jordan ambayo ina mamlaka ya kusimamia eneo hilo na udhibiti wa upatikanaji wake.**

**Waziri wa mambo ya nje wa nchi kadhaa za Kiislamu, ikiwemo Saudi Arabia, Egypt, Jordan, Pakistan na Indonesia, pia wamelaani vikwazo vinavyozuia Waislamu na Wakristo kufanya ibada katika mji wa Jerusalem.**

شوّال

HABARI MASHARIKI YA KATI

MAHMOUD NYAMGUMA

# Kinachofanywa na Israel kwa Wapalestina ni udhalimu



Nchi kadhaa za Kiislamu zikiongozwa na Saudi Arabia zimelaani Israel kwa kuweka vikwazo vinavyodaiwa kuzuia uhuru wa kuabudu katika mji mtakatifu wa Jerusalem, zikisema hatua hiyo ni ukiukwaji wa haki za msingi za kidini, Arab News wameripoti.

Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, Pakistan, Uturuki, Indonesia, Qatar, Jordan, Misri na Falme za Kiarabu wamesema kuzuia Waislamu kufika katika Msikiti wa Al-Aqsa ni "uchokozi wa wazi" unaoweza kuongeza mvutano wa kisiasa na kidini katika eneo hilo.

Hatua ya Israel kuwazuia Waislamu kuingia katika eneo la Al-Haram Al-Sharif imetajwa kuwa ya nadra kutokea katika miongo ya hivi karibuni. Takwimu kutoka mashirika ya haki za binadamu zinaonesha kuwa zaidi ya Wapalestina 50,000 hukusanyika kila wiki kwa ibada katika msikiti wa Al-Aqsa, lakini idadi hiyo hupungua kwa zaidi ya asilimia 60 wakati wa vikwazo vya kijeshi.

Shinikizo la kimataifa, likiwemo kutoka Vatican na Umoja wa Ulaya, lilimlazimu Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, kubadili uamuzi huo na kuruhusu ibada kuendelea wakati wa wiki takatifu, ingawa wachambuzi wanasema hatua hiyo haijgusi kiini cha mgogoro wa uhuru wa kuabudu kati ya Israel na Wapalestina.

Wakati huo huo, nchi hizo nane za Kiislamu zimekosoa pia sheria mpya ya Israel inayoruhusu adhabu ya kifo kwa Wapalestina wanaopatikana na hatia katika mahakama za kijeshi, zikisema inaweza kuongeza ukandamizaji na kuchochea mvutano zaidi.

# Kamati mpya ya kidini yapingwa na Waislamu Afrika Kusini

**Mtandao wa Waislamu Afrika Kusini (SAMNET) umepinga mpango wa Tume ya Haki za Utamaduni, Dini na Lugha (CRL) kuunda Kamati ya Kifungu cha 22 kusimamia shughuli za kidini, wakihofia kuhatarishwa uhuru wa dini uliolindwa kikatiba.**

**Kiongozi wa mtandao huo, Dkt. Faisal Suliman, amenukuliwa na tovuti ya habari ya IOL sheria zilizopo tayari zinatosha kudhibiti vitendo vya uhalifu ndani ya taasisi za kidini bila kuanzisha chombo kipya kinachoweza kuwa na mamlaka ya kupita kiasi.**

**Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kuna hofu kuwa kamati hiyo, ambayo awali inaonekana kulenga makundi ya Kikristo, inaweza kupanuliwa na kuathiri dini zote, ikiwemo Uislamu.**

**SAMNET inasisitiza kuwa vitendo kama udanganyifu wa kifedha, ukiukwaji wa sheria za kodi, na unyanyasaji wa kiimani vinaweza kushughulikiwa kupitia mifumo iliyopo ya vyombo vya sheria kama polisi na mahakama.**

**Aidha, mtandao huo umeonya kuhusu ongezeko la chuki dhidi ya Waislamu (Islamophobia), huku ripoti za mashirika ya haki za binadamu zikionesha ongezeko la chuki kwa takriban asilimia 20 maeneo ya mijini.**

MAHMOUD NYAMGUMA




# Mahakama Ufaransa yaruhusu mkusanyiko wa Waislamu baada ya zuio la miaka 7

**■ Mara ya mwisho mkutano huo ulifanyika mwaka 2019 kabla haujasimama kwa muda. Kabla ya kusitishwa, ulikuwa ukivutia zaidi ya washiriki 100,000 kila mwaka,**

Miaka saba baada ya kusitishwa, mkusanyiko mkubwa wa Waislamu nchini Ufaransa sasa unarejea kufanyika baada ya mahakama ya utawala kuruhusu tukio hilo kuendelea kama lilivyopangwa.

Kwa mujibu wa BBC News na France 24, tamasha hilo linalojulikana kama Mkutano wa Kila Mwaka wa Waislamu wa Ufaransa linatarajiwa kuvutia maelfu ya washiriki kutoka nchi mbalimbali za Ulaya.

Mara ya mwisho mkutano huo ulifanyika mwaka 2019 kabla haujasimama kwa muda. Kabla ya kusitishwa, ulikuwa ukivutia zaidi ya washiriki 100,000 kila mwaka, ukiwa moja ya majukwaa makubwa ya mijadala ya kidini, kitamaduni na kijamii kwa Waislamu barani Ulaya.

Hata hivyo, mafanikio ya kufanyika kwa mkutano huo hayakuja kirahisi.

Waandaaji walilazimika kusubiri hadi saa chache kabla ya ufunguzi ndipo mahakama ilipogeuza uamuzi wa polisi wa Paris waliokuwa wamepiga marufuku tukio hilo wakidai kuwa linaweza kuwa shabaha ya mashambulizi ya kigaidi au kusababisha vurugu kutoka kwa makundi ya mrengo mkali wa kulia.

Katika uamuzi wake, mahakama ilieleza kuwa ushahidi uliowasilishwa na mamlaka haukuthibitisha kuwepo kwa hatari ya moja kwa moja ya kiusalama.

Waandaaji wa mkutano huo kupitia chama cha Muslims of France (MF) walisema pia kuwa wameweka hatua za ziada za ulinzi ili kuhakikisha tukio hilo linafanyika kwa utulivu na usalama.

Ufaransa inakadiriwa kuwa na Waislamu kati ya milioni tano hadi sita, sawa na takribani asilimia 8 hadi 10 ya idadi ya watu. Kwa sababu hiyo, mkutano huo unaonekana kuwa jukwaa muhimu kwa jamii ya Kiislamu nchini humo, wakati mjadala kuhusu sera za serikali na uhuru wa kuabudu ukiendelea.

UKHTI FATIMA SS




# Vietnam na Kyrgyzstan zapambania nafasi katika soko la Halal duniani

Vietnam na Kyrgyzstan zimeanza kuongeza juhudi za kunufaika na soko la kimataifa la bidhaa na huduma za Halal, sekta inayokua kwa kasi na kuvutia uwekezaji wa mabilioni ya dola duniani.

Vietnam inalenga kupanua mauzo ya bidhaa zake katika soko hilo linalowahudumia zaidi ya Waislamu bilioni 1.9, sawa na takriban asilimia 25 ya watu duniani. Katika semina iliyofanyika Aprili 3 jijini Ho Chi Minh, Naibu Mkurugenzi wa Kituo cha Kukuza Biashara na Uwekezaji (ITPC), Ho Thi Quyen, alisema zaidi ya asilimia 63 ya Waislamu hutumia mara kwa mara bidhaa zenye uthibitisho wa Halal. Nchi za Baraza la Ushirikiano la Ghuba (GCC) pia huagiza kati ya asilimia 85 na 90 ya chakula wanachotumia, hali inayofungua fursa kwa wauzaji wa nje. Hata hivyo, ni takriban asilimia 0.2 tu ya makampuni ya Vietnam yenye vyeti vya Halal.




Wakati huo huo, Kyrgyzstan imeanzisha mfumo wa kidijitali wa kuomba vyeti vya Halal pamoja na matumizi ya misimbo ya QR ili kuongeza uwazi wa bidhaa. Nchi hiyo pia ilipitisha sheria ya "Halal Industry" mwaka 2024 ili kuimarisha udhibiti wa sekta hiyo.

Kwa mujibu wa wataalamu, matumizi ya bidhaa na huduma za Halal duniani yalifikia dola trilioni 2.43 mwaka uliopita na yanatarajiwa kuongezeka hadi dola trilioni 3.36 ifikapo mwaka 2028.

## AlHuda CIBE kusaidia Uzbekistan uanzishwaji mfumo fedha za Kiislamu

**Tashkent — Uzbekistan imechukua hatua muhimu katika kuanzisha mfumo wa fedha za Kiislamu baada ya kupitisha sheria mpya inayoweka msingi wa kisheria kwa shughuli za benki za Kiislamu nchini humo.**

**Sheria hiyo ilipitishwa Machi 27 na inatarajiwa kuanza kutumika miezi mitatu baada ya kuchapishwa rasmi. Mfumo huo mpya unaruhusu taasisi za fedha kutoa huduma zinazozingatia kanuni za Sharia kama uwekezaji wa kugawana faida, mikataba ya ushirikiano, mauzo ya malipo ya baadaye, mikataba ya malipo ya awali pamoja na ukodishaji wa Kiislamu (ijara).**

**Kwa mujibu wa mfumo huo, shughuli za benki ikiwemo fedha za Kiislamu zitafanywa na taasisi zilizopewa leseni na Benki Kuu ya Uzbekistan, huku leseni hizo zikitolewa bila muda maalum wa mwisho.**

**Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa nchi hiyo wa kupanua sekta ya fedha na kuvutia uwekezaji wa kimataifa pamoja na kuongeza ujumuishaji wa kifedha.**

**Wakati huohuo, AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics (AlHuda CIBE) imetangaza utayari wake kusaidia maendeleo ya sekta hiyo mpya kupitia mafunzo ya kitaalamu, ushauri wa Sharia, tafiti pamoja na ujenzi wa uwezo kwa taasisi za kifedha.**

## Benki za Kiislamu Bangladesh zaona fursa vijijini

**Dhaka — Benki za Kiislamu zimekuwa chaguo kuu kwa wakazi wengi wa vijijini nchini Bangladesh, zikisaidia kuongeza ujumuishaji wa kifedha na maendeleo ya uchumi katika maeneo ya pembezoni.**

**Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa na The Business Standard, wananchi wengi wa vijijini huchagua huduma za kifedha zinazozingatia kanuni za Kiislamu kwa sababu ya imani ya dini inayokataza riba (riba).**

**Mfumo wa benki za Kiislamu hutumia mbinu za kugawana faida na hasara kama mudarabah na musharakah, jambo linalowaruhusu watu kushiriki katika shughuli za kifedha bila kukiuka misingi ya dini yao.**

**Mbali na sababu za kidini, benki za Kiislamu zimefanikiwa kwa sababu zimepeleka huduma zao moja kwa moja vijijini ambako taasisi nyingi za kifedha zilikuwa hazijafika. Idadi ya matawi ya benki za Kiislamu katika maeneo ya vijijini imeongezeka kutoka 418 mwaka 2016 hadi kufikia zaidi ya 550 mwaka 2020, hatua iliyosaidia kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha.**

**Huduma za wakala wa benki pia zimepanua upatikanaji wa huduma hizi, huku maelfu ya vituo vidogo vya benki vikianzishwa katika maduka na masoko ya vijijini.**

**Utafiti unaonyesha kuwa mikopo na uwekezaji wa Kiislamu umechangia kupunguza umaskini wa vijijini kwa asilimia 8 hadi 10, huku pia ukisaidia wanawake wengi kupata mitaji ya kuanzisha biashara ndogo ndogo.**

## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS




# IsDB Institute yazindua kitabu kipya kuhusu misingi ya fedha za Kiislamu

Taasisi ya Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Institute – IsDBI) imetangaza kuchapishwa kwa kitabu kipya kiitwacho Essentials of Islamic Finance, kinachochambua kwa kina misingi ya fedha za Kiislamu na umuhimu wake katika kushughulikia changamoto za uchumi wa dunia.

Kitabu hicho kimeandikwa na Sami Al-Suwailem, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa IsDBI. Awali kilianza kama nyaraka ya kufundishia mwaka 2011, lakini sasa kimeboreshwa na kupanuliwa kwa kiasi kikubwa ili kujumuisha mifano, marejeo na maendeleo mapya ya kiuchumi duniani.

Kitabu kinaeleza kanuni kuu za mfumo wa fedha za Kiislamu, ikiwemo marufuku ya riba, umuhimu wa zaka na shughuli zisizo za kibiashara, pamoja na tahadhari dhidi ya gharar (hatari kubwa isiyoeleweka). Pia kinaeleza uhusiano wa moja kwa moja kati ya shughuli za kifedha na uchumi halisi. Kwa mujibu wa Profesa Bambang Susantono wa Bodi ya Wadhamini ya IsDBI, kitabu hicho kinaunganisha kanuni za kisheria za Kiislamu na fikra za kisasa za uchumi, na kinaweza kuwa rejea muhimu kwa wataalamu wa uchumi, watunga sera na watafiti wanaotaka kuelewa mfumo wa fedha za Kiislamu.




## Nigeria, IsDB zaimarisha ushirikiano wa maendeleo

**Lagos — Serikali ya Nigeria na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) zimetia saini makubaliano ya ushirikiano (MoU) yanayolenga kuimarisha maendeleo ya uchumi endelevu na kuboresha ustawi wa wananchi.**

**Makubaliano hayo yanalenga kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha sekta mbalimbali muhimu za maendeleo nchini humo. Ushirikiano huo umejengwa juu ya nguzo nne kuu ambazo ni maendeleo ya miundombinu kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi, maendeleo ya jamii na elimu, fedha bunifu zinazozingatia maadili pamoja na ushirikiano wa kikanda na wa nchi zinazoendelea.**

**Akinukuliwa na tovuti ya Fintech Futures jijini Lagos, Waziri wa Fedha wa Nigeria, Wale Edun, alisema nchi hiyo inalenga kupunguza utegemezi wa fedha za serikali na badala yake kuvutia uwekezaji kutoka sekta binafsi kupitia ushirikiano na taasisi za kimataifa kama IsDB.**

**Alisema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa kujenga uchumi wenye uwezo wa kustahimili misukosuko, unaojumuisha wananchi wengi na wenye ushindani katika soko la kimataifa.**

**Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Programu za Nchi katika IsDB, Anasse Aissami, alisema benki hiyo tayari imeidhinisha zaidi ya dola bilioni 2.32 kwa miradi mbalimbali nchini Nigeria, ikiwemo kilimo, nishati jadidifu na maendeleo ya uchumi wa halal.**

**Ushirikiano huo pia utachunguza matumizi ya fedha za Kiislamu kama sukuk katika kufadhili miradi ya maendeleo.**

شَوَّال

فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Nianze kufunga Sita za Shawwal au madeni ya Ramadhan?

**Swali: Je, inafaa kutanguliza kufunga sunna (saumu za hiari) kabla ya kulipa (qadha) saumu za Ramadhan? Kwa mfano, mtu afunge sita za Shawwal kisha alipe baadaye. Na je, riwaya iliyopokewa kutoka kwa Mama wa Waumini Aisha bint Abibakr (Allah amridhie) kuhusu kuchelewesha kulipa saumu hadi Shaaban ni sahihi au la? Tufafanulieni.**

**Jibu:** Swala hili lina ikhitilafu kati ya wanazuoni. Kauli iliyo na nguvu zaidi ni kwamba mtu aanze na kulipa (qadha) kwa sababu Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Atakayefunga Ramadhani kisha akaifuatisha na sita za Shawwal, basi ni kama amefunga mwaka mzima."

Ikiwa mtu hakukamilisha kufunga Ramadhan, vipi ataifuatisha na sita za Shawwal? Hivyo, anatakiwa kwanza akamilishe hiyo Ramadhan (kwa kulipa siku alizozikosa).

Mwanamke pia anapaswa kulipa siku alizoziacha za Ramadhan, kisha ndipo afunge sunna ikiwa ataweza. Asipoweza, basi hakuna dhambi juu yake, Alhamdulillah.

Kwa upande mwingine, wapo baadhi ya wanazuoni waliosema kuwa mtu anaweza kuanza na sunna kwa sababu muda wake ni mfupi na unaweza kupita, wakati kulipa (qadha) kuna muda mpana.

Kwa mtazamo wa wanazuoni wa kundi hili, hakuna ubaya kuanza na sita za Shawwal, au kufunga Jumatatu na Alhamisi, au siku ya Arafa na kadhalika; kisha akalipa madeni ya Ramadhan baadaye.

Ingawa kauli ya pili nayo ina uzito fulani wa kifiqhi, ni kauli ya kwanza ndiyo iliyo wazi zaidi na yenye nguvu kwa sababu faradhi ni muhimu zaidi.

Kadhalika, huenda mtu akapatwa na kifo au maradhi, hivyo ni bora aanze na jambo la lazima (qadha), kisha akipata nafasi ndio afunge sunna.

Ama kuhusu riwaya ya Aisha bint Abibakr (Allah amridhie), ni hadithi sahihi iliyopokelewa katika vitabu sahihi, ambapo alisema: "Nilikuwa na deni la saumu ya Ramadhan, na sikuweza kuilipa isipokuwa katika mwezi wa Shaaban, kwa sababu ya kujishughulisha (kumhudumia) Mtume (Allah amshushie rehema na amani)." Hata hivyo, haipaswi kudhani kwamba alikuwa akitanguliza sunna na kuacha faradhi. Hii ni kwa sababu alikuwa pia akiacha kufunga sunna kwa sababu ya kumhudumia Mtume (Allah amshushie rehema na amani), basi ni wazi zaidi kwamba asingetanguliza sunna juu ya faradhi.

Kwa ujumla, kitendo chake hakitthibitishi kuwa alikuwa akifunga sunna kabla ya kulipa qadha. Hakusema kwamba alikuwa akifanya hivyo, bali alisema tu alikuwa akichelewesha qadha kwa sababu ya majukumu yake kwa Mtume.

Inaonekana kwamba Aisha bint Abibakr hakuwa akifunga sita za Shawwal wala sunna nyingine wakati bado ana deni la qadha, na huenda alikuwa akichelewesha zote kwa sababu hiyo. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Je, inaruhusiwa kufunga siku sita za Shawwal kwa mtu ambaye bado anadaiwa siku za kulipa (qadha) za Ramadhan? Na je, siku hizo zifungwe mfululizo au inaruhusiwa kuzitenganisha?**

**Jibu:** Kufunga siku sita za Shawwal ni miongoni mwa sunna zilizothibiti kutoka kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Sunna hii imepokewa katika hadithi kadhaa, miongoni mwazo ni, mosi, kutoka kwa Abu Ayyub al-Answariy kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Atakayefunga Ramadhan kisha akaifuatisha na sita za Shawwal, basi hiyo ni kama kufunga mwaka mzima." [Muslim na wengineo].

Pili, kutoka kwa Thawban, kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani), amesema: "Atakayefunga Ramadhan na sita baada ya Idd el Fitri, hiyo ni kukamilisha mwaka mzima; mema hulipwa mara kumi." [Ibn Majah na An-Nasaiy, na ni hadithi sahihi].

Tatu, imepokewa kutoka kwa Thawban katika riwaya nyingine kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "Kufunga Ramadhan ni kama miezi kumi, na kufunga siku sita ni kama miezi miwili, hivyo hiyo ni sawa na kufunga mwaka mzima." [Riwaya sahihi].

Kwa msingi huo, hakuna ubishi kuwani sunna kufu nga siku sita za mwezi wa Shawwal. Hata hivyo, aliye na deni la qadha ya Ramadhan, lililo bora kwake ni kuanza kulipa (qadha) kwanza, kisha afunge sita za Shawwal, kwa sababu qadha ni faradhi na sunna haiwezi kutangulia faradhi.

Vilevile, si lazima kufunga siku sita mfululizo; bali inaruhusiwa kuzifunga kwa kutenganisha siku hizo.

Kadhalika, ikiwa atazifunga katika siku za Jumatatu na Alhamisi, hiyo ni vizuri zaidi, na atapata pia fadhila ya kufunga siku hizo mbili. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Watanzania tutafakari ushiriki wetu ibada ya Hijja

Kuingia kwa mwezi wa Shawwal ni ishara ya kukamilika kwa ibada ya swaumu ya Ramadhan, ambayo ni nguzo ya nne ya Uislamu. Mbali na kutekeleza funga ya siku sita za Shawwal (ambayo ni sunna iliyosisitizwa – Mu'akkadah), mwezi huu pia ni kipindi muhimu cha maandalizi ya ibada adhimu ya Hijja.

Hata hivyo, inasikitisha kuona Waislamu wengi nchini wanashindwa kuiwajibikia ibada ya Hijja licha ya kuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Wanasahau kuwa Hijja ni ibada ya faradhi kama zilivyo sala, zaka na nyinginezo.

Allah Mtukufu anasema katika Qur'an: "Na kwa ajili ya Allah imewajibika watu watekeleze Hijja katika Nyumba hiyo kwa awezae kuiendea. Na atakayekanusha (mwenye kuweza na asihiji), basi hakika Allah si muhitajii kwa walimwengu." [Qur'an, 3:97].

Aya hii ni miongoni mwa dalili zinazoonesha uzito wa kuacha au kukanusha amri ya Hijja. Kwa msingi huo, wanazuoni wamekubaliana kuwa Hijja ni miongoni mwa ibada za faradhi, na mwenye kuikanusha anakuwa amekufuru.

Ni kwa sababu hiyo, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwahimiza Waislamu kuharakisha kutekeleza ibada ya Hijja aliposema: "Harakisheni kwenda Hijja, kwani hakika mmoja wenu hajui atapatwa na nini huko mbele." [Ahmad, Bayhaqi na Ibn Majah].

Aidha, maimam Abu Hanifa, Ahmad na Malik, pamoja na baadhi ya wanafunzi wa Imam Shafi wamesema: "Hijja inamuwajibikia kila mtu mara tu anapokuwa na uwezo," wakirejea hadith hiyo.


## Sababu za mwamko mdogo wa Hijja

Katika utafiti mdogo tulioufanya, imebainika kuwa ushiriki mdogo wa Waislamu wa Tanzania katika ibada ya Hijja unatokana na mchanganyiko wa sababu za kiuchumi, kielimu na kijamii.

Miongoni mwa sababu hizo ni baadhi ya Waislamu kujiwekea malengo ya kwenda Hijja watakapofikia umri wa uzee, kwa kisingizio kuwa bado hawajamaliza starehe na anasa za dunia. Haya ni mawazo duni, kwani hakuna anayejua muda wake wa kuishi hapa duniani.

Vilevile, wapo wanaohofia Hijja zao kupotea bure baada ya kuzitekeleza, kwa kuwa bado wanatarajia kurejea katika maovu waliyokuwa wakiyafanya awali.

Sababu nyingine ni ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa ibada ya Hijja. Waislamu wengi hawapati mafunzo ya kina kuhusu namna ya kujiandaa kifedha na kiroho kwa ajili ya ibada hii.



Matokeo yake, wengi huiona Hijja kuwa ni ibada ya matajiri pekee, ilhali ni wajibu unaohitaji mipango ya muda mrefu. Aidha, baadhi ya watu huweka vipaumbele vingine kama kujenga nyumba bora, kununua magari ya kifahari au kuwekeza katika biashara kabla ya kufikiria Hijja.

Kwa kiasi kikubwa, mambo haya ndiyo yanachangia Waislamu wengi kushindwa kutekeleza ibada hiyo muhimu. Inasikitisha kuona kuwa, tangu uhuru Tanzania haijawahi kupeleka mahujaji hata 5,000 kwa mwaka, licha ya Serikali ya Saudi Arabia kuipa nafasi 20,000 za mahujaji kila mwaka. Hata hivyo, tunaamini ikiwekwa mikakati madhubuti ya kifedha, elimu na uratibu bora, inawezekana kuongeza idadi ya Waislamu wanaotekeleza ibada hii.

Mikakati hiyo ni pamoja na Masheikh, wanazuoni na walinganiaji kutumia nafasi walizonazo kutoa faida na kuwahamasisha vijana kuhusu umuhimu wa nguzo ya Hijja. Hatua hiyo itasaidia vijana kuondokana na dhana ya kusubiri uzee ndipo wakahiji, na pia itaongeza idadi ya mahujaji na kuhakikisha wajibu wa Hijja unatekelezwa kwa wakati muafaka.

Kwa kuzingatia dhima na wajibu wa ibada ya Hijja, ni muhimu kutambua kuwa anayewajibika kwenda Hijja ni yule mwenye uwezo wa kiafya na kifedha, lakini hiyo haimaanishi lazima awe tajiri.

Kwa kifupi, anayewajibika kwenda Hijja ni yule mwenye afya njema na uwezo wa kumudu gharama za safari ya kwenda na kurudi Makka pamoja na matumizi ya njiani, na kuacha mahitaji ya kutosha kwa familia yake wakati akiwa Hijja. Mwenye uwezo huo, Hijja inakuwa imemuwajibikia.

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803



# Vitisho vya Trump na yaliyojificha nyuma ya pazia

**Katika toleo lililopita, tulishuhudia Rais Donald Trump wa Marekani akitoa wito kwa mataifa mengine kuingilia kati vita kati ya nchi yake na Israel dhidi ya Iran kwa lengo la kusaidia kufunguliwa tena Mlango – Bahari wa Hormuz. Leo tunakamilisha sehemu iliyosalia. Sasa endelea...**

# Vitisho vya Trump na yaliyojificha nyuma ya pazia



Rais Trump alikosolewa vikali na Seneta wa Chama cha Democratic, Chris Murphy, ambaye aliandika kwenye mitandao ya kijamii: "Siwezi kuelezea kwa undani zaidi jinsi Iran inavyoulinda Mlango – Bahari, lakini inatosha kusema kuwa kwa sasa hawajui namna ya kuufungua tena kwa usalama."

Kauli hiyo ilitolewa kufuatia hatua ya utawala wa Trump kuwasilisha mipango yake kwa Bunge la Marekani katika kikao cha faragha.

Nalo gazeti la New York Times lilimkosoa Trump kwa kusema: "Februari 18, Rais Trump alipopima uwezekano wa kuanzisha mashambulizi ya kijeshi dhidi ya Iran, Waziri wa Nishati, Chris Wright alimweleza mwandishi aliyekuwa akimhoji kuwa hakuwa na wasiwasi kwamba vita hiyo ingeweza kuvuruga usambazaji wa mafuta kutoka Mashariki ya Kati na kuyumbisha masoko ya nishati duniani."

Tathmini hiyo ilitokana na shambulio la pamoja la Marekani na Israel dhidi ya Iran mwezi Juni 2025, lililojulikana kama 'Vita ya Siku 12'.

Gazeti hilo liliongeza: "Hata wakati wa mashambulizi ya Israel na Marekani dhidi ya Iran, Bw. Wright alisema kulikuwa na usumbufu mdogo katika masoko, ambapo bei ya mafuta ilipanda na baadaye kushuka tena."

Katika muktadha huo, Donald Trump alilazimika kuwasiliana na Rais wa Urusi, Vladimir Putin akitarajia kupata msaada wake.

Msaidizi wa Rais wa Urusi, Yury Ushakov, alisema Machi 9, 2026 kwamba: "Donald Trump alimpigia simu Vladimir Putin kujadili masuala kadhaa muhimu yanayohusiana na hali ya sasa ya kimataifa. Umakini maalumu uliwekwa kwenye mzozo wa Iran. Mazungumzo hayo yalikuwa makini, ya wazi na yenye kujenga."

Kwa mujibu wa taarifa hizo, Rais wa Urusi aliwasilisha mambo kadhaa ya kuzingatia yaliyolenga kufanikisha suluhu ya haraka ya kisiasa na kidiplomasia kuhusu mzozo wa Iran, ikiwa ni pamoja na mawasiliano aliyofanya na viongozi wa mataifa ya Ghuba, Rais wa Iran, Masoud Pezeshkian, pamoja na viongozi wa nchi nyingine kadhaa.

Kutokana na mazungumzo hayo, Trump alitangaza kuwa yalikuwa chanya, na kwamba Marekani inaweza kufikiria kupunguza vikwazo vilivyowekwa kwenye mafuta ya Urusi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Majid Takht–Ravanchi alisema: "Tunasisitiza kuwa hakuna uchokozi zaidi unaopaswa kufanywa ili kufanikisha usitishaji wa mapigano. Nchi kadhaa, ikiwemo China, Urusi na Ufaransa zimewasiliana nasi kuhusu usitishaji huo."

Inaonekana Marekani inaelekea kufungua njia kupitia Urusi au mataifa mengine kwa ajili ya mazungumzo na Iran ili kumaliza vita hiyo – njia ambayo inaweza kuinusuru katika hali ngumu na wakati huo huo kuifanya ionekane mshindi.

Hata hivyo, matumaini ya Israel katika mashambulizi ya haraka iliyoyafanya kwa kushirikiana na Marekani kuwaua viongozi wa Iran, kuwa yangesababisha kuanguka kwa utawala wa nchi hiyo yamegonga mwamba.

Walitarajia hatua hiyo ingemaliza vita kwa haraka, lakini hali imekuwa tofauti. Badala yake walikumbana na majibu makali kutoka Iran, yaliyosababisha uharibifu mkubwa kutokana na mashambulizi ya makombora ndani ya Israel na maeneo mengine ya Mashariki ya Kati.

Aidha, inaonekana Iran ina uwezo hata wa kuikomboa Palestina, lakini haikuliweka hilo kama lengo lake kuu. Ushawishi wa Marekani uliifanya Iran kuepuka kuingia moja kwa moja kijeshi katika mzozo wa Palestina.

Kwa upande mwingine, Iran iliamini kuwa kujikurubisha kwa Marekani kungeisaidia kuhifadhi na kuimarisha utawala wake, kupanua ushawishi wake wa kikanda, pamoja na kuiwezesha kutengeneza silaha za nyuklia na kuendeleza sekta yake ya makombora.

Hata hivyo, Marekani ilionekana kuwa na mkakati wa kupunguza matarajio hayo na kuigeuza Iran kuwa taifa dhaifu.

شوّال

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Huu ndiyo Uislamu aliotuachia Mtume

Licha ya kuwapo kwa tofauti nyingi za kimila, desturi na lugha baina ya watu wa mataifa mbalimbali, jambo moja lililopo ndani ya kila nafsi ya mwanadamu ni kumtambua Muumba wake na kujisalimisha kwake kwa kumtii na kumuabudu.

Ni kweli kabisa kwamba kila mtu ana uhuru wa kuchagua dini anayoona inafaa na yenye manufaa kwake, lakini dini pekee anayoiridhia Mwenyezi Mungu ni Uislamu, kama anavyosisitiza: "Na yeyote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu, basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa miongoni mwa waliopata hasara (kubwa kabisa)." [Qur'an, 3:85].

Ili kuepuka hasara hiyo, ipo haja kwa kila mwanadamu kufuata dini sahihi aliyokuja nayo Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Ninaposema dini sahihi namaanisha mila, desturi, kanuni, misingi, miiko na utamaduni wa dini asili (Uislamu) aliyouelekeza Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Mtume ametuachia Uislamu sahihi uliyojengwa juu ya misingi ya imani na matendo mema, unaomwezesha mwanadamu kupata furaha hapa duniani na kesho Akhera.

Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa, wapo miongoni mwetu wanaoifanyia mzaha dini, wakimkufuru Mwenyezi Mungu na kupuuza ibada zake, licha ya kufikiwa na ubainifu na dalili ya kuthibiti kwa ibada hizo.

Kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Kiislamu, Muislamu anatakiwa kutenda mema kwa nia safi na moyo mkunjufu, pamoja na kuzingatia mwenendo wa Mtume (rehema na amani imshukie).

Qur'an inasema: "Na wala hawakuamrishwa ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini." [Qur'an, 98:5]. Ukiitafakari kwa kina aya hii, utaona kuwa wale wanaojisalimisha kwa Mola wao, wakatekeleza ibada kwa uaminifu na kuonesha mwenendo bora, watafanikiwa duniani na Akhera, na watapata kheri kubwa siku ya Kiyama.

## Hakuna Uislamu bila tauhidi

Inajulikana wazi kuwa msingi mkuu wa Uislamu ni tauhidi, yaani kumwamini Allah Mmoja bila kumshirikisha na chochote. Huu ndiyo ujumbe mkuu alioubeba Mtume Muhammad katika maisha yake yote ya Utume.

Mtume aliwahimiza watu kuacha ibada za sanamu na badala yake wamwabudu Muumba wao kwa utii na unyenyekevu. Kwa maana hiyo, tauhidi si kauli ya mdomo pekee, bali ni imani inayodhihirika katika vitendo, ikiwa ni pamoja na kumuabudu Mwenyezi Mungu, kumtegemea Yeye pekee, kumuogopa na kumpenda kwa dhati.

## Ni upi Uislamu sahihi wa kufuata

Uislamu sahihi ni ule unaotekelezwa kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'an na Sunna, kwa uaminifu na uelewa wa wema waliotangulia.

Kwa mantiki hiyo, Muislamu anatakiwa kuishi kwa kufuata Qur'an na Sunna bila kupotosha yaliyomo ndani ya viwili hivyo au kuyageuza kwa matakwa binafsi.

Uislamu unasisitiza uadilifu katika biashara, heshima kwa wazazi, wema kwa ndugu, jamaa na majirani, pamoja na huruma kwa viumbe wote.

Maadili haya ni sehemu muhimu ya ibada, kwani Uislamu hauishii kwenye ibada ya sala msikitini pekee bali unajumuisha mwenendo mzima wa maisha ya kila siku.

Aidha, Uislamu unahimiza umoja na kuepuka mifarakano. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwausia Waislamu kushikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu na kujiepusha na migawanyiko isiyo na msingi.

Katika jamii mbalimbali duniani, migogoro mingi hutokana na tofauti za mitazamo au maslahi binafsi. Kwa kuliona hilo, Mtume aliondoa ubaguzi uliokuwepo katika jamii ya Kiarabu na kusisitiza usawa wa binadamu wote.

Kauli yake maarufu katika khutba ya kuaga inaonesha wazi kuwa hakuna ubora wa Mwarabu juu ya asiye Mwarabu isipokuwa kwa uchamungu. Aidha, Mtume alihimiza elimu kwa wanaume na wanawake, akisisitiza kuwa elimu ni nuru inayomwongoza mwanadamu katika maisha ya dunia.

Ni muhimu kutambua kwamba Uislamu haupingani na maendeleo, bali unahimiza maendeleo yanayoendana na maadili ya dini na haki.

Hata hivyo, changamoto kubwa katika zama za leo ni kupotoshwa kwa mafundisho sahihi ya Uislamu kutokana na tafsiri potofu, misimamo mikali, au kupuuza vyanzo sahihi vya dini.




Baadhi ya watu huongeza mambo ambayo hayapo katika mafundisho ya Mtume, huku wengine wakipunguza au kupuuza mafundisho muhimu ya dini, hali inayosababisha mkanganyiko na kuharibu taswira halisi ya Uislamu.

Waislamu wengi huona ugumu kufuata sharia za Uislamu kutokana na upungufu wa elimu ya dini. Wasichokijua ni kwamba Uislamu ni dini ya wastani (wasatwiyyah) inayozingatia uwiano katika kila jambo la maisha ya mwanadamu, kuanzia ibada, maadili, usawa, haki na elimu.

Ili kurejea katika Uislamu sahihi, ni muhimu kwa Waislamu kujifunza dini yao kwa kina kutoka katika vyanzo sahihi na kwa wanazuoni wanaoaminika. Pia, ni muhimu kuzingatia maadili ya Kiislamu katika maisha ya kila siku na kuepuka misimamo mikali au ya kupindukia.

Waislamu tuna wajibu wa kujifunza, kuelewa na kuutekeleza Uislamu kwa usahihi ili kufikia mafanikio ya hapa duniani na Akhera tuendako.

شوّال

MAKALA MAALUM



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Hukumu ya kuoa mwanamke mjamzito

**Hakika sharia tukufu ya Kiislamu ni kamilifu na inajumuisha kila nyanja ya maisha, ikifanya kazi katika kila zama na kila mahali. Miongoni mwa ukamilifu wake ni uwezo wake wa kujibu kila suala na kutoa hukumu ya kisharia kwa kila tukio.**

**Hili linafanyika kupitia vyanzo vyake vikuu ambavyo ni Qur'an, Sunna, Ijmaa (makubaliano ya wanazuoni), na Qiyas (ulinganifu wa kisharia). Hivyo basi, Uislamu haukuacha jambo lolote, dogo wala kubwa bila kulibainisha – ama kwa ufafanuzi wa kina au kwa maelezo ya ujumla.**

Katika safu hii, leo tunajadili hukumu zinazomhusu mwanamke aliyepata ujauzito kwa njia ya zinaa. Hili linaonesha namna ambavyo Uislamu umeipa familia umuhimu mkubwa, ukihimiza uimara wake kwa kuzingatia misingi ya dini na maadili mema.

Sababu ya hilo ni kwamba, familia ndiyo msingi wa jamii. Familia zikiwa imara na safi, jamii nayo hunufaika na kuwa bora; lakini zinapodhoofika na kutawaliwa na maovu, jamii nzima hupotoka.

Miongoni mwa mambo ambayo Uislamu unayazingatia kwa umakini mkubwa ni kulinda nasaba ya mtoto aliye tumboni. Kwa msingi huo, Uislamu umeharamisha ndoa ya mwanamke mjamzito hadi ajifungue. Ni muhimu kufahamu kuwa baadhi ya mambo yameharamishwa kwa sababu ya madhara yake kwa jamii.

Miongoni mwa mambo hayo ni uzinzi na kila kinachopelekea katika zinaa, kama vile kuchanganyika kiholela kati ya wanaume na wanawake, kukaa faragha mwanaume na mwanamke ambao si maharimu, mwanamke kutoka nje ya nyumba yake bila hijab, na mambo mengine yanayofanana na hayo. Yote haya yameharamishwa kwa sababu yanafungua milango ya kutenda maovu makubwa.

Mwanazuoni Ibn Qayyim (Allah amrehemu) amesema: "Kwa kuwa malengo hayawezi kufikiwa isipokuwa kwa kupitia njia na sababu zinazoelekea kuyafikia, basi njia hizo hufuata hukumu ya malengo hayo. Hivyo, njia zinazopelekea mambo ya haramu na maasi huzuiwa kulingana na uzito wa madhara yake, na zile zinazopelekea utiifu na ibada huruhusiwa na kupendekezwa kwa kadri zinavyofikisha kwenye malengo hayo."

Suala linalojadiliwa hapa ni je, sharia ya Kiislamu inaruhusu kumuoa mwanamke aliyepata ujauzito kwa njia ya zinaa? Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu wametofautiana mitazamo kuhusu suala hili.

## Kauli ya kwanza

Kwa mujibu wa madhehebu ya Malik na Hanbali, ndoa ya mwanamke mwenye ujauzito wa zinaa ni batili na haramu. Hivyo, mwanamke huyo hawezi kuolewa hadi ajifungue. Aidha, kama anaishi na mwanaume bila ndoa lakini hajapata ujauzito, pia atalazimika kukaa eda.

Baadhi ya wanazuoni wameeleza kuwa mwanamke huyo anatakiwa kusubiri (istibra') kwa hedhi tatu au miezi mitatu, na wengine wamesema hedhi moja inatosha kwa kuwa si mke halali.

Hoja yao ni kauli ya Allah Mtukufu: "Na wanawake wajawazito muda wao (wa eda) ni mpaka wajifungue mimba zao." [Qur'an, 65:4]. Aya hii inaonesha kuwa mwanamke mjamzito anatakiwa kukamilisha eda yake kwa kujifungua, bila kujali ujauzito umetokana na ndoa halali au zinaa.

Aidha, kwa mujibu wa qiyas (ulinganifu wa kisharia), kama hairuhusiwi kufunga ndoa na mwanamke aliyepata ujauzito kwenye ndoa ya halali (baada ya kutalikiwa au kufiwa), basi pia hairuhusiwi kwa aliyepata ujauzito kwa njia ya zinaa.

## Kauli ya pili

Kauli ya pili inasema, inaruhusiwa kufunga ndoa na mwanamke mzinifu – awe mjamzito au la, na hana sharti la kusubiri eda. Kwa mujibu wa kauli hii, mwanamke mwenye ujauzito wa zinaa anaweza kuolewa kabla ya kujifungua, hata kama ujauzito umetokana na mwanaume mwingine.

Huu ni mtazamo wa Imam Shafi na Ibn Hazm. Hoja yao ni kauli ya Allah Mtukufu: "Mmeharamishiwa mama zenu, na mabinti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na mama zenu wadogo, na mabinti wa ndugu zenu wa kiume na wa kike..." [Qur'an, 4:23].

Aya hii imewataja wanawake walioharamishwa kuwaoa, kisha Allah akabainisha kwa kusema: "...na mmehalalishiwa wengineo wasiokuwa hao..." [Qur'an, 4:24].

Maana yake ni kwamba wanawake wasiokuwa katika orodha ya waliotajwa kuwa ni haramu inaruhusiwa kuwaoa. Kwa hiyo, mwanamke aliyepata ujauzito kwa zinaa hayumo katika waliokatazwa, hivyo ndoa yake ni halali.

## Kauli ya tatu

Kauli ya tatu inaeleza kuwa, inaruhusiwa kufunga ndoa na mwanamke aliyepata ujauzito wa zinaa, uliotokana na mwanaume anayetaka kumuoa au mwingine. Hata hivyo, kwa mujibu wa madhehebu ya Hanafi, mwanamke huyo hatakaa eda.

Na ikiwa tayari ni mjamzito, ndoa inasihi kufungwa lakini hairuhusiwi kumuingilia hadi ajifungue. Hoja yao inatokana na kauli ya Allah Mtukufu: "...na mmehalalishiwa wengineo wasiokuwa hao..."

Katika aya hii, mwanamke mzinifu hakutajwa katika wale waliokatazwa kuwaoa, hivyo inaruhusiwa kumuoa na ndoa yake ni sahihi.

Katazo la kumuingilia mwanamke mwenye ujauzito wa zinaa linatokana na hadith ya Mtume (rehema na amani zimshukie) inayosema: "Haipasi kwa mtu anayemwamini Allah na Siku ya Mwisho kumwaga (maji ya uzazi) juu ya mbegu aliyootesha mwingine." [Abu Daudi].

## Kauli sahihi

Kwa mtazamo wangu, ndoa ya mwanamke mwenye ujauzito wa zinaa ni haramu hadi ajifungue. Hii ni kwa sababu Uislamu unalinda familia na nasaba, hivyo ni lazima mwanamke huyo asubiri hadi ajifungue, kisha ndipo aruhusiwe kufunga ndoa.

شَوَّال

KALAMU HURU

SEHEMU YA 3

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Kujidhibiti-Siri ya mafanikio baada ya Ramadhan

**Miongoni mwa mafunzo makubwa na yenye thamani ambayo Muislamu alifunzwa ndani ya mwezi wa Ramadhan namna ya kujidhibiti – yaani alijengewa uwezo kuizuia nafsi isifuate kila kinachotamanisha, na badala yake kuiongoza kufuata yale yanayompendeza Mwenyezi Mungu. Kujidhibiti ni nini? Ni hali ya mtu kuwa na uwezo wa kusimamia matamanio yake, hisia zake, na matendo yake kwa kuzingatia mipaka ya dini. Ni kusema "hapana" pale nafsi inapovutiwa na jambo lisilofaa, na kusema "ndiyo" pale inapohitajika kufanya jambo jema, hata kama ni gumu.**

Katika mwezi wa Ramadhan, Muislamu alijifundisha nidhamu hii kwa njia ya vitendo. Kwa muda wa siku nzima, alijizuia kula, kunywa, na mambo mengine yaliyo halali nje ya kipindi cha Ramadhan.

Ikiwa aliweza kujizuia na vitu halali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi inapaswa kuwa rahisi zaidi kujizuia na yale yaliyo haramu.

Hekima ya funga inaonekana hapa katika kumjenga Muislamu aweze kuiongoza nafsi yake badala ya kuongozwa nayo; hasa tukizingatia kuwa, aghlab, matatizo mengi ya mwanadamu hutokana na kushindwa kudhibiti nafsi yake.

Baada ya Ramadhan kuisha, changamoto halisi huanza. Hakuna tena mazingira yale ya kiroho yanayomzunguka mtu kila mahali; misikiti kujaa, watu wengi kufunga, na hali ya ibada kuwa ya pamoja. Sasa Muislamu anabaki peke yake na maamuzi yake.

## Je, ataendelea kujidhibiti?

Katika maisha ya kila siku, kuna vishawishi vingi vinavyomzunguka mwanadamu: kuangalia mambo yasiyofaa, kusema maneno yasiyofaa, kula kupita kiasi, kupoteza muda katika mambo yasiyo na faida, na mengine mengi. Bila ya kujidhibiti, ni rahisi sana mtu kuingia katika mtego wa maasi.

Muislamu aliyefundishwa na Ramadhan anatakiwa kuwa na misingi imara ya nidhamu ya nafsi; ajifunze kupanga muda wake vizuri, kudhibiti matumizi yake, na kuongoza maisha yake kwa malengo yenye maana.

Moja ya njia muhimu ya kujidhibiti ni kuwa na malengo ya wazi. Mtu asiye na malengo huwa rahisi kufuata matamanio ya nafsi yake, lakini yule mwenye malengo —hasa ya kidini na kimaisha—atajitahidi kujiepusha na mambo yanayompotezea muda na nguvu.

Aidha, kujidhibiti kunahitaji juhudi za makusudi na sio jambo linalokuja lenyewe tu. Muislamu anapaswa kujizoesha taratibu, kama vile kupunguza muda wa mambo yasiyo na faida, kujiwekea ratiba ya ibada, na kujilazimisha kufanya mambo mema hata kama nafsi haipendi mwanzoni.

Vilevile, mazingira yana mchango mkubwa katika kujenga au kubomoa nidhamu ya nafsi. Ni muhimu kwa Muislamu kujiepusha na mazingira mabaya na kujisogeza karibu na watu wema watakaomsaidia kubaki katika mstari ulio sahihi.

Kujidhibiti pia kunahusiana moja kwa moja na mafanikio ya maisha ya dunia. Watu wengi waliofanikiwa katika nyanja mbalimbali ni wale walio na nidhamu ya hali ya juu katika maisha yao. Hivyo basi, Ramadhan haimjengi Muislamu kwa ajili ya Akhera tu, bali pia kwa ajili ya mafanikio ya dunia.

Kwa hakika, mtu anapoweza kuidhibiti nafsi yake, anakuwa huru kweli. Hawi tena mtumwa wa matamanio yake, bali anakuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu, na huo ndio uhuru wa kweli.

Hivyo basi, ni jukumu la kila Muislamu kuhakikisha kuwa mafunzo ya kujidhibiti aliyoyapata katika Ramadhan hayaishii ndani ya mwezi huo, bali yanaendelea kuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku.


Lakini pamoja na kujidhibiti, jambo jingine muhimu ni uhusiano wa karibu na Qur'an, ambalo tutalizungumza katika makala inayofuata, chini ya anuanim "Qur'an Mwongozo wa Maisha Baada ya Ramadhan."

Humo, tutaeleza jinsi Muislamu anavyoweza kuendelea kushikamana na Qur'an, hata baada ya Mwezi Mtukufu kuondoka.

شوّال

# TUJIFUNZE
## AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama



# AI si uchawi, ni asilimia 100 sayansi

**Licha ya umaarufu wake, bado kuna watu wengi wanaona Akili Mnemba (AI) kama kitu cha ajabu au uchawi. Ukweli ni tofauti kabisa. AI ni sayansi inayotumia data na kanuni za kihisabati kufanya kompyuta ziweze kujifunza na kufanya maamuzi.**

**Kwa maneno mengine, AI ni programu ya kompyuta inayoweza kufanya baadhi ya kazi ambazo zamani zilihitaji akili ya binadamu—kama kutambua picha, kuelewa lugha au kutatua matatizo.**

### AI tayari ipo katika maisha yetu

AI si teknolojia ya baadaye bali ipo tayari katika maisha yetu ya kila siku.

Unapotumia ramani kwenye simu kutafuta njia fupi ya kwenda kazini, au unapopata mapendekezo ya video kwenye YouTube, mara nyingi kuna mfumo wa AI unaofanya kazi nyuma ya pazia.

AI huchambua taarifa zako za matumizi—kama video ulizotazama—kisha unapendekeza vitu vinavyofanana na ladha yako. Hivyo basi, hata kama hatulitambui mara moja, AI tayari imekuwa sehemu ya maisha ya kila siku. Simu janja zimejaa mifumo ya AI.

Achilia mbali usaidizi wa ramani na mapendekezo ya video; AI inafanya kazi kubwa za kitaaluma ikiwemo kusaidia madaktari kugundua magonjwa mapema, kusaidia wakulima kupata mavuno bora, na kusaidia serikali kupanga huduma za umma kwa ufanisi zaidi. Katika elimu pia, AI inaweza kusaidia wanafunzi kujifunza kwa njia inayolingana na uwezo wao binafsi.

### Msingi wa AI: data na algoritimu

Ili kuelewa AI vizuri, ni muhimu kuelewa vitu viwili vinavyoifanya ifanye kazi: data na algoritimu.

Data ni taarifa ambazo mfumo wa AI hutumia kujifunza. Taarifa hizi zinaweza kuwa picha, maandishi, sauti au namba; wakati algoritimu, kwa upande mwingine, ni kanuni za mahesabu—seti ya maelekezo yanayoeleza kompyuta jinsi ya kuchambua data hiyo. Kama data ni viungo vya chakula, algoritimu ni mapishi yanayoelekeza jinsi ya kupika chakula hicho.

Kwa mfano, kama kampuni inataka kutengeneza mfumo wa AI wa kugundua barua pepe za utapeli, wataipa kompyuta maelfu ya barua pepe—zile halisi na zile za utapeli. Kisha algoritimu itachambua tofauti kati ya aina hizo mbili. Baada ya muda, mfumo unaweza kujifunza kutambua barua pepe za utapeli hata kama hajawahi kuziona hapo awali.

### AI hujifunza kama mwanafunzi

Njia kuu ambayo AI hujifunza huitwa 'kujifunza kwa mashine' (machine learning). Hii ni mbinu inayoruhusu kompyuta kujifunza kutoka kwenye data badala ya kupewa sheria zote moja kwa moja.

Fikiria mfano rahisi: kama unataka kufundisha mtoto kutambua paka, unaweza kumuonyesha picha nyingi za paka. Kadri anavyoona picha nyingi, ndivyo anavyoanza kutambua sifa za paka—kama masikio, macho au manyoya.

AI hufanya kitu kinachofanana. Ikipewa picha nyingi za paka, mfumo unaweza kujifunza kutambua paka katika picha mpya. Kwa sababu hiyo, AI mara nyingi huhitaji data nyingi sana ili kufanya kazi vizuri.

### Kwa nini AI inaweza kufanya makosa?

Licha ya uwezo wake mkubwa, AI si mkamilifu. Wakati mwingine inaweza kutoa majibu yasiyo sahihi au hata kutengeneza taarifa ambazo hazipo.

Katika mifumo ya kisasa ya AI—hasa inayotumia lugha kama ChatGPT—tatizo hili wakati mwingine huitwa "hallucination." Mfumo unaweza kutoa majibu yanayoonekana ya kitaalamu lakini si sahihi kabisa.

Hii hutokea kwa sababu AI imeundwa kutambua mifumo ya lugha na data, si lazima kuthibitisha ukweli wa kila taarifa.

Mfano uliotolewa na watafiti unaonyesha kwamba mtu anaweza kuuliza AI kuhusu dawa mpya ya ugonjwa fulani, na mfumo ukataja dawa ambazo zinaweza kuwa halisi au hata kutokuwepo kabisa.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 2

# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika toleo lililopita tumeona kwa muhtasari kizazi cha Israil (Ya'qoub) kilivyoanza kupoteza mwelekeo, hali iliyosababisha kuwa duni na dhalilifu.**

**Mtawala wa mwisho wa Misr (Fir-aun) alikichukia zaidi kizazi cha Israil, akawatesa na kuwaua magerezani. Lakini kubwa zaidi, aliagiza vijana wao wa kiume wauawe na wasichana wao waachwe hai.**

**Pia, tuliona kwamba katika kipindi hiki kigumu alizaliwa Mtume Musa bin Imran (amani ya Allah imshukie) na kuishi.**

**Mama yake Musa aliogopa sana taarifa za kujifungua zisije kuvuja na kuwafikia askari wa Fir-aun, na kusababisha mwanawe kuchinjwa kama walivyochinjwa mamia ya wenzake.**

**Mama Musa akawa alifikiri sana namna ya kumficha mwanawe asionwe na askari wa Fir-aun. Hapo mama huyu akapokea ilhamu (ujumbe) kutoka kwa Mola wake unaomuelekeza atengeneze sanduku linalozuia maji kuingia, amuweke Musa kisha aliweke sanduku hilo kwenye mto Nile.**

**Allah alimhakikishia mama Musa kwamba atamrejeshea mtoto wake na atakuwa mtu mkubwa wa miujiza.**

**Qur'an inasema: "Tukamfunulia mama yake Musa (tuliutia ufahamu moyo wake) ya kwamba, mnyonyeshe; na utakapomhofia basi mtie mtoni, na usiogope wala usihuzunke, kwani sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume." [Qur'an, 26:7].**

**Mama yake alifikiri sana hatma ya mwanawe iwapo atamtosa mtoni. Mto utalilibeba sanduku alimomhifadhi mwanawe mpaka wapi? Humo atakuaje? Atafikia mikononi mwa nani? Atanyonyeshwa na nani?**

**Yote haya yalipita moyoni mwa mama huyo mwenye uchungu wa uzazi, lakini aliuzingatia vyema wah-I (maelekezo) na kumtegemea Allah. Akamtosa mtoto wake kwenye mto.**

## Musa kuokolewa

Sanduku lilielea-elea na kupita kwenye fukwe karibu na kasri la kifahari la Fir-aun. Watu wa Fir-aun wakalichukua na kumpelekea mkuu wao, ambaye aliamrisha sanduku lifunguliwe.

Linafunguliwa! Tahamaki wanamkuta mtoto wa kiume akiwa salama, anatabasamu. Watu waliokuwepo, akiwemo Fir-aun mwenyewe na mkewe, walishangaa sana.

Katika hali ya kutaka kumtambua mtoto, wengine wakaotea kwa kusema, "Bila shaka huyu ni mtoto wa Kiisrail" na kisha wakashauri: "Apitishiwe hukumu ile ile ya kuuliwa."

Qur'an inaeleza: "Watu wa Fir-aun wakamuokota ili awe adui kwao na huzuni. Bila shaka Fir-aun na Hamana na majeshi yao walikuwa wakoseaji sana." [Qur'an, 28:8].

## Musa kunusurika kuuawa

Allah Aliyetukuka akaingiza huruma na mapenzi ya ajabu katika moyo wa mke wa Firaun, akamuomba mumewe mtoto asiuliwe, badala yake wamfanye wa kwao na huenda atakuwa wa manufaa na kuwasaidia hapo baadae. Hapa inadhihiri wazi kanuni isemayo "Alitakalo Allah huwa."

Tuirejee tena Qur'an: "Na mke wa Fir-aun akasema (kumwambia mumewe) atakuwa kiburudisho cha moyo kwangu na kwako, msimuuwe huenda atatunufaisha au tumpange kuwa mtoto (wetu) na hali hawatambui (kuwa atakuwa adui wao)." [Qur'an, 28:9].

Basi hivi ndivyo Mtume Musa aliyetolewa kuja kuiangusha serikali dhalimu alivyoingia na kulelewa katika jumba la mfalme huyo mtesaji, jabari mwenye kibri, huku ulinzi mkali mitaani nyumba kwa nyumba ukiendelea. Allahu Akbar!

Allah alitaka Fir-aun amlee mtu atakayeondoa utawala wake kwa mikono na gharama zake ndani ya kasri lake!

Kwa hiyo, tuseme kwamba, miujiza ya Mtume Musa ilianza kuonekana tangu akiwa mchanga. Musa akawa mtoto mzuri, pambo la nyumba yao, kila mtu anampenda, kila mtu anambusu. Mapenzi ya kila mtu yalifuata mapenzi ya yule Malkia.

## Nani amnyonyeshe mtoto

Lakini swali, ni je mtoto atanyonyeshwa na nani ilhali bado yungali mchanga?

Malkia aliwaita wamama kadhaa, mmoja baada ya mwengine. Kila mmoja alifanya juhudi kubwa ya kumbembeleza mtoto ili amridhishe Malkia na kupata malipo ya unyonyeshaji, lakini Musa alikataa kunyonya na akaendelea kulia kilio, tena cha kwikwi!

Mtoto aliwashuhulisha watu na kuwa nukta ya gumzo. Mtoto mzuri lakini ajabu mbona hataki kunyonya!?

## Simazi ya Mama wa Musa

Hayo yakijiri kwenye kasri; huku moyo wa mama wa Nabii Musa ulijaa hofu, simanzi na akatingwa na mawazo juu ya mtoto wake.

Qur'an inasema: "Moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu (hauwazi ila kuhusu mwanawe tu) alikuwa karibu kudhihirisha (siri ya kuwa yule ni mtoto wake) kama tusingeutia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa wenye kuamini (ahadi za Mwenyezi Mungu).

"Na akamwambia dada yake (dada wa Musa), 'Mfuatilie (fuata njia aliyochukuliwa na maji) basi akamwangalia kwa mbali bila wao kujua.

"Na tulimharamishia wanyonyeshaji tangu mwanzo (makusudi ili tumrejeshe kwa mama yake) dada yake akawaambia, 'Je nikuenesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu na pia watakuwa wema kwake?' (wakakubali, akawaelekeza kwa mama yake ambaye ndiye mama wa Musa)." [Qur'an, 28:10-12].

*Itaendelea inshaAllah*

شوّال

MAKALA YA AFYA
0764 101 018

SEHEMU YA 2



**DKT.**
**Omar A. Kasuwi**
**Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!**
**Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)**

# Ratiba rahisi ya kila siku kwa watoto wasiopenda kula

**Wazazi wengi hukumbana na changamoto moja inayofanana: mtoto kutokula vizuri. Wengine huchagua chakula wanachotaka kula, wengine hula kidogo sana, na wengine hukataa kabisa vyakula fulani. Hali hii inaweza kuwafanya wazazi kuwa na wasiwasi kuhusu afya na ukuaji wa watoto wao.**

**Hata hivyo, wataalamu wa lishe ya watoto wanasema kwamba mara nyingi tatizo hili linaweza kupunguzwa kwa kuweka utaratibu rahisi na wa utulivu wa kula nyumbani. Badala ya kumlazimisha mtoto kula au kufanya meza ya chakula iwe chanzo cha msongo, wazazi wanaweza kutumia mbinu zinazosaidia mtoto kukuza hamu ya kula kwa njia ya kawaida.**

**Hapa chini ni ratiba rahisi ya kila siku inayoweza kusaidia watoto wanaokula kwa shida.**

## Mosi: Chakula kiwe muda maalumu

Weka muda maalumu wa chakula na vitafunwa. Watoto hunufaika sana wanapokuwa na utaratibu unaoeleweka. Wataalamu wanashauri chakula na vitafunwa vitolewe kwa muda ule ule kila siku. Hii humsaidia mtoto kuzoea ratiba na mwili wake huanza kujifunza wakati wa kuhisi njaa.

Ni muhimu pia kuepuka mtoto kula kidogo kidogo muda wote wa siku. Tabia ya kula kila mara bila mpangilio, inayojulikana kama 'grazing', inaweza kumfanya mtoto asijisikie njaa wakati wa chakula kikuu. Ratiba iliyo wazi humsaidia mtoto kujiandaa kisaikolojia na kimwili kwa wakati wa kula.

## Pili: Aanze kwa kifungua kinywa chenye afya

Mzazi anashauriwa aanze siku kwa kumpa mtoto kifungua kinywa chenye afyam yaani mlo kamili. Kifungua kinywa ni mlo muhimu kwa watoto. Baada ya kulala usiku kucha, mwili wa mtoto unahitaji nguvu mpya ili kuanza shughuli za siku. Kifungua kinywa kinachojumuisha maziwa, matunda na nafaka kinaweza kusaidia kuamsha hamu ya kula na kuongeza nguvu.

Mfano rahisi unaweza kuwa glasi ya maziwa, kipande cha tunda kama ndizi au chungwa, pamoja na mkate au uji. Mlo wa asubuhi unaosaidia mtoto kupata nguvu huongeza uwezekano wa kula vizuri katika milo inayofuata.

## Tatu: Mpe kidogo kidogo

Toa kiasi kidogo cha chakula mara kwa mara. Wazazi wengi hujaribu kumpa mtoto sahani iliyojaa wakiamini kwamba ataimaliza. Lakini kwa watoto wanaokula kwa shida, njia hii inaweza kuwa na matokeo tofauti. Sahani iliyojaa inaweza kumfanya mtoto ahisi shinikizo na hatimaye kukataa kula.

Njia bora ni kumpa mtoto kiasi kidogo cha chakula. Akimaliza na bado ana njaa, anaweza kuomba zaidi. Mbinu hii humfanya mtoto ajisikie huru na hupunguza mvutano unaoweza kutokea wakati wa kula.

## Nne: Epuka skrini wakati wa kula

Katika familia nyingi, televisheni au simu hutumika kama njia ya kumshawishi mtoto kula. Hata hivyo, wataalamu wanasema matumizi ya skrini wakati wa kula yanaweza kupunguza umakini wa mtoto kwa chakula.

Ni vizuri kuunda mazingira tulivu ya kula—bila televisheni, simu au michezo ya video. Wakati wa kula unaweza pia kuwa nafasi nzuri ya mazungumzo ya familia. Mazingira haya humsaidia mtoto kula kwa utulivu na kutambua ladha ya chakula.

## Tano: Msifu mtoto kwa jitihada

Msifu mtoto kwa Juhudi, si kiasi cha chakula. Wazazi wengine huweka shinikizo kwa watoto wao kumaliza sahani nzima ya chakula. Lakini mbinu hii inaweza kumfanya mtoto ahusishe chakula na hofu au shinikizo.

Badala yake, ni bora kumpongeza mtoto kwa kujaribu chakula kipya au kumaliza hata sehemu ndogo. Sifa ndogo kama "umejaribu vizuri" au "hongera kwa kuonja chakula hiki" zinaweza kuongeza hamasa ya mtoto kula zaidi polepole.

Kwa ujumla, watoto wengi hupitia kipindi fulani cha kuwa wachaguaji wa chakula. Hali hii si ya kudumu na mara nyingi hubadilika kadiri wanavyokua. Kwa kuweka ratiba rahisi, mazingira tulivu na mtazamo wa uvumilivu, wazazi wanaweza kumsaidia mtoto kukuza tabia nzuri ya kula bila msongo wa mawazo.

Hatimaye, lengo si kumlazimisha mtoto kula sana mara moja, bali kumsaidia kujenga uhusiano mzuri na chakula kwa muda mrefu.



MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Sanaa ya kumwambia mtoto "Hapana" bila kumuumiza kihisia

Katika malezi ya watoto, wazazi mara nyingi hulazimika kusema "hapana." Mtoto anaweza kutaka kitu kisichofaa, kufanya jambo hatari au kuvuka mipaka ya nidhamu ya familia

Changamoto kwa wazazi wengi si kusema "hapana" yenyewe, bali jinsi ya kuisema bila kuharibu uhusiano wa kihisia na mtoto. Wataalamu wa saikolojia ya watoto wanaeleza kuwa njia ya mawasiliano ya mzazi inaweza kuathiri sana jinsi mtoto anavyojithamini na kuelewa mipaka ya maisha.

Kwa mtazamo wa saikolojia ya malezi, kusema "hapana" kwa ukali au kwa hasira kunaweza kutoa matokeo ya haraka, lakini mara nyingi huacha athari za muda mrefu. Mtoto anaweza kujenga hofu, upinzani au kujisikia kukataliwa. Ndiyo maana wataalamu wanashauri wazazi kujifunza sanaa ya kusema "hapana" kwa njia chanya—njia inayoweka mipaka wazi lakini pia inalinda hisia za mtoto.

## Nguvu ya maneno katika malezi

Watoto hujifunza kuhusu dunia kupitia maneno na tabia za wazazi wao. Maneno ya kukataza kama "acha," "usifanye," au "hapana kabisa" yanaweza kuonekana rahisi, lakini yakitumika mara kwa mara bila maelezo yanaweza kumfanya mtoto ajisikie kukosolewa kila wakati. Hii haimaanishi wazazi waache kuweka mipaka. Kinyume chake, watoto wanahitaji mipaka ili kujifunza nidhamu na usalama. Hata hivyo, tofauti kubwa ipo katika jinsi mzazi anavyowasilisha katazo. Mtoto akielewa sababu ya katazo na kuhisi kuwa mzazi anamheshimu, huwa na uwezekano mkubwa wa kukubali maelekezo.

## Kusikiliza mtoto kwanza

Njia mojawapo ya kumkatalia mtoto bila kumuumiza kihisia ni kuanza kwa kumsikiliza kwa makini. Kabla ya kusema hapana, mzazi anaweza kuuliza mtoto anataka nini na kwa nini. Kusikiliza huku kunamfanya mtoto ajisikie kuthaminiwa.

Kwa mfano, mtoto akitaka kucheza nje wakati wa kufanya kazi za shule, mzazi anaweza kusema: "Ninaelewa unataka kucheza sasa, lakini kwanza tumalize kazi ya shule." Kauli kama hii inaonesha kwamba mzazi amesikia ombi la mtoto, hata kama hatakubali mara moja.

## Kutumia ishara na mawasiliano yasiyo ya maneno

Si kila katazo linahitaji maneno makali. Wataalamu wa malezi wanashauri wazazi kutumia ishara za mawasiliano yasiyo ya maneno kama kuangalia mtoto machoni, kutikisa kichwa au kuonyesha kwa mkono. Mara nyingi ishara hizi zinatosha kumkumbusha mtoto mipaka bila kuzua mgongano wa maneno.

## Kutoa maelekezo yanayoendana na umri wa mtoto

Njia ya kumkatalia mtoto pia inapaswa kuendana na umri wake. Watoto wadogo mara nyingi hawahitaji maelezo marefu; badala yake wanahitaji kuelekezwa kwa jambo lingine. Mzazi anaweza kutumia mbinu ya kumvutia mtoto katika shughuli nyingine ili kumsaidia kuondoka katika jambo lisilofaa.

Kwa watoto wakubwa au vijana, mazungumzo yanaweza kuwa ya kina zaidi. Mzazi anaweza kuwahimiza kufikiria matokeo ya maamuzi yao—kwa mfano, kuangalia faida na hasara za kitendo wanachotaka kufanya. Hii huwasaidia kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina na kuwajibika.

## Badala ya amri, tumia maombi ya heshima

Wazazi wengi hutumia amri kali bila kutambua athari zake. Kubadilisha amri kuwa ombi la heshima kunaweza kubadilisha kabisa mazingira ya mawasiliano nyumbani. Badala ya kusema "acha mara moja," mzazi anaweza kusema, "tafadhali acha hilo sasa."

Maneno kama "tafadhali" na "asante" yanaweza kuonekana madogo, lakini yanafundisha mtoto umuhimu wa heshima na mawasiliano mazuri.

Weka muda maalum wa kucheza na mtoto

Wataalamu wa malezi pia wanashauri wazazi kuweka muda maalum wa kucheza na watoto wao. Wakati huu mtoto anaweza kujieleza kwa uhuru na kufanya makosa bila kuhukumiwa. Hii hujenga uhusiano wa karibu kati ya mzazi na mtoto.

Mtoto anayehisi kuwa mzazi wake anampa muda na kumsikiliza huwa tayari zaidi kukubali mipaka inapowekwa.

## Mtazamo wa Uislamu katika malezi

Katika Uislamu, malezi ya watoto yanahimizwa kufanywa kwa upole, subira na huruma. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mfano bora wa upendo kwa watoto. Alikuwa akiwachezea, kuwabeba na kuwasikiliza kwa upole.

UKHTI FATIMA SS



# Aina 8 ya mawazo yanayoharibu hali ya moyo wako

Mara nyingi tunapozungumzia afya ya akili, tunafikiria mambo makubwa kama msongo wa mawazo au matatizo ya maisha. Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia wanasema kwamba mara nyingi hali yetu ya kihisia huathiriwa na namna tunavyofikiri. Kuna mifumo fulani ya mawazo ambayo inaweza kuharibu hali ya moyo, kupunguza kujiamini na hata kuathiri mahusiano yetu na watu wengine.

Mifumo hii huitwa cognitive distortions—yaani mitazamo potofu ya kufikiri. Hapa chini ni baadhi ya mifumo nane ya mawazo inayoweza kuharibu hali ya mtu bila yeye kujitambua.

## Mosi: Kujihukumu vibaya

Kuweka lebo kwa nafsi 'labeling' ni katika mawazo mabaya yanayoharibu moyo wako. Hii hutokea pale mtu anapofanya kosa moja kisha anajiwekea lebo ya kudumu. Kwa mfano, mtu akifanya makosa kazini anaweza kusema, "Mimi ni mtu asiye na uwezo."

Badala ya kuona tukio kama kosa la muda, linaloweza kurekebishika katika majaribio ya baadae mtu huanza kujiona nafsini vibaya kabisa, kama mtu aliyeshindwa na asiyefaa. Mtazamo huu hupunguza kujiamini na huweza kumfanya mtu akate tamaa mapema.

## Pili: Kudharau mafanikio yako mwenyewe

Watu wengine wanapofanikiwa jambo fulani, hulipunguza umuhimu wake. Mtu anaweza kufaulu mtihani au kufanikisha mradi lakini akasema, "Hiyo si kitu, mtu yeyote angeweza kufanya." Tabia hii huondoa uwezo wa kufurahia mafanikio.

Hali hii ya kufanya mafanikio kitu cha kawaida, kisicho na thamani maalumu, hukujengea wewe mwenyewe mtazamo wa kujiona huna thamani na kuharibu moyo wako.

## Tatu: Dhana mbaya wengine wanavyokuona

Kudhani unajua mawazo ya wengine (mind-reading) ni katika mambo ya kuhujumu furaha yako. Katika hali hii, mtu huanza kudhani anajua kile ambacho watu wengine wanafikiria kuhusu yeye. Kwa mfano, unaweza kudhani kuwa mtu anayekutazama kimya anakudharau au hakupendi, wakati pengine alikuwa anafikiria jambo lingine kabisa. Tatizo la mtazamo huu ni kwamba hujenga wasiwasi usio wa lazima.

## Nne kujitabiria mabaya

Kutabiri mabaya kabla hayajatokea (fortune-telling) ni jambo jingine linaloharibu moyo wako. Hii hutokea kwa kuamini kuwa mambo yataenda vibaya hata kabla hayajatokea. Kwa mfano, mtu anaweza kusema: "Nikiomba kazi hii sitapata," au "Jaribio hili litaishia kushindwa." Mawazo ya aina hii huondoa motisha na mara nyingi humfanya mtu asijaribu kabisa.

## Tano: Kubena mambo kibinafsi

Kujichukulia kila jambo kibinafsi (personalization) hutokea pale mtu anapodhani kuwa kila tukio lina uhusiano wa moja kwa moja na yeye. Kwa mfano, rafiki akionekana kimya unaweza kudhani amekukasirikia, wakati huenda alikuwa na matatizo yake binafsi. Mtazamo huu unaweza kusababisha migogoro au huzuni isiyo ya lazima.

## Sita: Hitimisho la jumlajumla

Kufanya hitimisho la jumla kutokana na tukio moja (overgeneralizing ni kosa linalofanywa na wengi wetu na kutuingiza katika hali ya kukata tamaa, kuchukia kundi la watu na kupoteza motisha.

Katika hali hii, mtu huchukua tukio moja hasi kisha analifanya kuwa sheria ya kudumu. Kwa mfano, mtu akikataliwa katika maombi ya kazi moja anaweza kusema, "Mimi huwa sipati kazi kabisa." Hii hujenga mtazamo wa kukata tamaa na kumfanya mtu ashindwe kuona fursa nyingine.

## Saba: Kuamini hisia zako bila ushahidi

Hali mbalimbali zinazotutokea - ikiwemo mwongozo wa moyo, historia ya maingiliano na watu na ushahidi wa mazingira - zinatufanya tuwe na hisia (emotional reasoning) kuhusu mambo tofauti tofauti. Hisia hizi zinaweza kuwa za kweli au sio za kweli.

Tatizo linakuja pale baadhi yetu tunapoamini kuwa hisia zetu siku zote lazima ziwe za kweli, na si vinginevyo. Kwa mfano, mtu anaweza kusema: "Ninahisi sina uwezo, kwa hiyo lazima niwe kweli sina uwezo." Tatizo ni kwamba hisia zetu wakati mwingine huathiriwa na hofu au msongo wa mawazo, si ukweli halisi.

Mbaya zaidi ni pale hisia zako zinapokuelekeza kuwa umerogwa, fulani hakupendi, kitu fulani hukiwezi hivyo kukifanya kazi bure – hutafanikisha.

NA UKHTI FATIMA



# Kwa nini elimu yetu bado inazalisha wasaka ajira, si watengeneza ajira?

**Moja ya changamoto kubwa katika mfumo wetu wa elimu ni matarajio tunayowajengea wanafunzi tangu wakiwa wadogo. Mara nyingi vijana hufundishwa kwamba kusoma ni njia ya kupata ajira nzuri na mshahara mnono. Hili limekuwa kama falsafa isiyoandikwa ya elimu yetu: soma sana, pata cheti, ajiriwe, kisha uanze maisha mazuri.**

Lakini uhalisia wa soko la ajira ni tofauti kabisa. Kupata ajira yenyewe tayari ni changamoto kubwa, achilia mbali ile yenye mshahara mkubwa. Wakati matarajio haya makubwa yanapokutana na uhalisia wa soko la ajira lenye nafasi chache, ndipo mfadhaiko kwa vijana wengi huanza.

Tatizo haliko tu kwenye matarajio ya kijamii, bali pia katika muundo wa mitaala yetu. Kwa muda mrefu, mfumo wa elimu umejikita zaidi katika kumtengeneza kijana anayeweza kuajiriwa badala ya kumjenga kijana anayeweza kujiajiri. Msisitizo mkubwa umekuwa katika kumwandaa mwanafunzi kuwafurahisha waajiri, badala ya kumfundisha namna ya kuunda ajira yake mwenyewe.

Matokeo yake ni hali ya kushangaza kidogo katika jamii. Katika mazingira mengi, vijana ambao hawakuendelea sana na masomo—kwa mfano waliomaliza darasa la saba au kidato cha nne—mara nyingi wanaonekana kuwa wabunifu zaidi katika kutafuta njia za kujipatia kipato. Wanaingia mapema katika shughuli za kiuchumi, wanajaribu biashara ndogo ndogo, na wanajifunza kwa vitendo namna ya kujitegemea.

Ni nadra kusikia vijana wa darasa la saba au kidato cha nne wanaandamana kudai ajira serikalini. Licha ya kukosa ajira rasmi, wengi wao wanaendelea kuishi kwa kujitafutia kipato kupitia kazi mbalimbali.

Hali hii inaonekana hata ndani ya familia. Katika baadhi ya nyumba unaweza kukuta vijana wawili: mmoja hakusoma sana na aliingia mtaani mapema, na mwingine amehitimu elimu ya juu. Mara nyingi yule aliyeingia mapema katika shughuli za maisha anaonekana kuwa mbunifu zaidi katika kutafuta njia za kuendesha maisha.

Hii haimaanishi kwamba elimu haina thamani. Kinyume chake, elimu ni muhimu sana. Lakini changamoto iko katika aina ya elimu tunayotoa na mtazamo tunaoujenga kwa vijana.

Ndiyo maana mitaala ya ngazi ya diploma imekuwa na mvuto fulani kwa sababu mara nyingi hujumuisha somo la ujasiriamali. Somo hili huwasaidia vijana kuanza kufikiria kujiajiri kama njia halali ya maisha, badala ya kuona ajira kama chaguo pekee.

Ni kweli kwamba juhudi zimeanza kufanyika kubadilisha mitaala ili kusisitiza zaidi elimu ya vitendo. Hata hivyo, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha elimu inawajenga vijana wenye uwezo wa kuunda fursa badala ya kusubiri fursa.

Moja ya mapendekezo muhimu ni kuongeza ushiriki wa watu kutoka sekta binafsi katika ufundishaji. Walimu wengi waliopo shuleni wana uzoefu wa kitaaluma lakini si lazima wawe na uzoefu mkubwa wa kufanya biashara au kuanzisha miradi. Vijana wanahitaji pia kuona mifano halisi ya watu waliothubutu na kufanikiwa katika maisha ya kiuchumi.

Watu kutoka sekta binafsi wanaweza kuwahamasisha wanafunzi kwa uzoefu wao wa vitendo. Badala ya kuwahubiria tu nadharia, wanaweza kuwaonyesha njia halisi za kufikiria fursa na kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Miaka ya nyuma kulikuwa na ushauri uliotolewa na viongozi wa serikali kwamba vijana waende kupata ujuzi katika vyuo vya mafunzo ya ufundi. Ingawa baadhi ya watu waliuchukulia ushauri huo kama mzaha, ukweli ni kwamba ulikuwa na msingi mzuri.

Ujuzi wa vitendo katika fani kama ufundi wa magari, useremala, umeme au udereva unaweza kuwa chanzo cha kipato cha uhakika.

Si jambo la ajabu leo kukutana na kijana mwenye shahada anayemwomba nauli ndugu yake aliyemaliza darasa la saba na anayefanya kazi ya bodaboda. Wakati kijana aliyesoma anaendelea kulalamika kuhusu kukosa ajira, ndugu yake ambaye hakujifungia katika fikra za "ajira ya ofisini" anaendelea kujenga maisha yake.

Wapo vijana wanaoendesha familia zao kupitia shughuli kama bodaboda, kuuza genge, udereva wa daladala au ufundi wa magari. Wameoa, wamejenga na wanasomesha watoto wao kupitia kazi hizo. Tatizo kubwa ni kwamba baadhi ya vijana waliohitimu elimu ya juu wanaona kazi kama hizi hazilingani na hadhi ya elimu yao.

Bahati mbaya, hata elimu inayolenga kuandaa watu kwa ajira ina changamoto zake. Waajiri wengi hulalamika kuwa vyuo vinazalisha wahitimu ambao hawajaiva vya kutosha kuingia moja kwa moja katika mazingira ya kazi.

Hii inaonyesha wazi kwamba changamoto si elimu yenyewe, bali namna tunavyoitengeneza na kuitumia. Mfumo wa elimu unaojenga ubunifu, ujuzi wa vitendo na ujasiriamali unaweza kuwa chombo kikubwa cha maendeleo ya uchumi.

Swali muhimu tunalopaswa kujiuliza ni hili: tunataka elimu itengeneze watafuta ajira, au watengeneza ajira?